# *Waebrania, Mlango Wa Sita* [3]

Habari za asubuhi, wapendwa. Ni majaliwa kuwapo hapa. Na—na kutimiza utangulizi huu mkuu kutoka kwa mchungaji wetu hakika kungehitajika maisha manyofu, sivyo? Kwa hiyo tunamhimidi Bwana kwa ajili ya nguvu Zake zote kuu za uponyaji na rehema Zake ambazo ametupa sisi katika miaka hii yote.

Sasa nina matangazo machache ya kutangaza. Mojawapo ni, sisi, Ndugu Woods na Ndugu Roberson, na tunataka kuwashukuru ninyi nyote kwa ajili ya kutuombea, kuwa na safari ya salama. Tulikuwa na wakati mzuri sana; tulisafiri tu kwa siku nne na nusu, naamini, na tukarudi tena salama. Bwana alitubariki.

506 Sasa, tunatangaza ya kwamba Ndugu Graham Snelling, ufufuo wake, unaendelea, huko mwi—mwishoni mwa Barabara Kuu ya Brigham, kwenye ninii...jijini hapa. Na usiku wa Jumatano hii ijayo...Ninataka kuondoka kesho, baada ya ibada ya mazishi ya mtu mmoja nitakayemtangaza hivi punde. Tutawajulisha Jumatano usiku. Tunataka kwenda katika tume, sote, huko kumtembelea Ndugu Graham kabla hajafunga ibada yake kule. Nasi tutajaribu kuwa na kanisa zima pamoja, tukiweza, na twende kama tume kukutana, kuwa pamoja na Ndugu Graham katika moja ya ibada zake.

507 Na, sasa, alasiri ya leo kwenye—kwenye nyumba ya mzishi huko Charlestown, kuna Bi—Bibi Colvin, ambaye wakati mmoja alihudhuria kanisa hili hapa miaka mingi iliyopita, umri wa miaka sabini na minne, aliyaacha maisha haya jana kwenda kuwa pamoja na Bwana Yesu. Na mazishi yake yatahubiriwa Jumatatu, na Kasisi Bw. McKinny, alikokuwa, hapo awali, mchungaji wa kanisa la Kimethodisti huko—huko Port Fulton kwa miaka mingi, ambaye alikuwa ni rafiki wao msiri. Nami yabidi nimsaidie, Jumatatu, kwenye, ninaamini ni saa saba na nusu, kwenye—kwenye kanisa dogo huko Charlestown, Indiana. Na ninyi nyote marafiki wa familia ya Colvin mngeninii, najua, sasa mngethamini kwa ujasiri mdogo tu ama kuninii...kupeana mikono kidogo. Kwa maana sisi sote tunajua mtu unajisikiaje kwenye jambo hilo, sisi ambao tumepitia mambo hayo, kwenye mabonde, sisi wenyewe, na kujua jinsi inavyomaanisha kupoteza rafiki fulani. Na kwa hiyo sisi...Yeye yuko kwenye—kwenye kanisa hilo dogo sasa, huko Charlestown, Indiana. Kama mkienda huko alasiri ya leo, mbona, jambo hilo lingethaminiwa na familia ya Colvin, nina hakika. Wengi wa ndugu zao wangali wanahudhuria hapa maskanini. Nimewafungia ndoa, nimewazika, nimewabatiza, karibu familia yao yote. Na kwa

hiyo Bw. Grayson, ambaye alikuwa ni jirani yetu papa hapa, ndiye mtayarishaji wa mazishi kule.

508 Na halafu kuna jambo hili, usiku wa leo, Bwana akipenda, mahali tulipoachia asubuhi ya leo, tutajaribu kuanzia hapo usiku wa leo, katika somo hili kuu ambalo tunasoma sasa. Na halafu nafikiri hayo yalikuwa ndiyo matangazo, kadiri mi—mi ni—ni nijuavyo. Na Jumatano hii ijayo usiku, sasa, tutatangaza usiku tutakaokwenda kule kuwa pamoja na Ndugu Graham.

509 Nasi tunawakaribisha wageni wote malangoni mwetu. Nasi tuna furaha kuwa nanyi hapa asubuhi ya leo, na tunaomba ya kwamba Mungu atawabariki mno, kwa wingi, leo kwa ajili ya kukusanyika huku.

510 Ndugu Cox ndiyo kwanza aniambie ya kwamba vyombo vya mfumo wa kupaaza sauti havikuwa vikifanya kazi vizuri sana wakati huu. Labda ni ninii, huenda ikawa ni kwa sababu ya hali ya hewa, kuna unyevunyevu mwingi kule kwenye hizo spika. Nazo si nzuri sana, kwanza, kwa hiyo huenda ikawa ndiyo sababu.

511 Nikiwa ninamwona dada fulani ameketi hapa ambaye ninamjua, Dada Arganbright. Mimi . . . Hili si jambo zuri na—na adabu nzuri, kuuliza jambo hili, lakini je! una habari zozote kutoka kwa Ndugu Arganbright tangu alipokuwa kule. Nina hamu sana ya kusikia kutoka kwake mapema tuwezavyo. Yeye yuko huko Uswisi na Ujerumani, kwenye mkutano kule pamoja na Ndugu Tommy Hicks na Paul Cain. Kama ukipata kusikia, Dada Ruth, nipashe habari mara moja, upesi tu uwezavyo.

512 Sasa, maskani hii ndogo haina uanachama, bali tuna ushirika. Hatuna kanuni ya imani ila Kristo, hatuna sheria ila upendo, hatuna kitabu ila Biblia. Hicho ndicho Kitabu pekee tukijuacho, na ndicho kitu pekee tujuacho, kama kitu tulicho nacho. Kwa kuwa Damu ya Yesu Kristo hutusafisha na dhambi zote, tuna ushirika sisi kwa sisi, kila mtu.

513 Nilikuwa nikihakiki, asubuhi ya leo, kwa baadhi yenu ninyi watu huenda mmemsikia huyo ndugu akiomba. Huyo alikuwa ni Mkatoliki, kwa hiyo, ama hapo kwanza alikuwa ni Mkatoliki. Na tuna watu wa aina mbali mbali wanaokuja hapa. Sasa hivi tu nimepata majaliwa, dakika chache zilizopita, kupeana mkono na ndugu wa Kimenoni ambaye anaketi hapa ndani. Basi kutoka kwa Wamenoni, kutoka kwa Wamethodisti, kutoka kwa Wabaptisti, na Wakatoliki, ama yeyote atakaye, na waje. Nasi tunashiriki pamoja kwenye baraka za Neno la Mungu. Walioko sasa wameketi ni Mashahidi wa Yehova na watu wa aina mbalimbali, tuliona madhehebu mbalimbali.

514 Nilikuwa ninapenda (vema, ningali ninapenda) sehemu za Magharibi. Ninapenda farasi na ng'ombe. Nilikuwa tu nimelelewa shambani, na mimi—napenda hilo. Na tulikuwa tukiwakusanya ng'ombe, nami ningeenda pamoja nao. Na

tulikuwa na ua msepetuko. Sijui kama ninyi watu wa Mashariki mnajua ua msepetuko ni kitu gani, ama hamjui. Ni wakati mnapowaweka ng'ombe m—msituni, wana ua wa kuwazuia wasitawanyike vile walivyoliita, warudi kwenye maranchi. Wangekula nyasi, sehemu ambako wanakuza nyasi kwa ajili ya malisho ya msimu wa baridi. Na halafu huko juu mlimani, wana nyua msepetuko pia, ambapo wanawatenganisha majike mengi mbali na madume, na kadhalika. Unaitwa ua msepetuko. Lakini ua msepetuko mkuu ni pale mwangalizi anaposimama wakati ng'ombe wanapopita.

515 Na sasa nimewahi kuketi kule, kwa siku nyingi, kwenye matandiko yangu ya farasi, na kuwaangalia wakati ng'ombe walipopita pale. Kulikuwa na aina zote za chapa zilizoingia. Kulikuwa na baadhi walioitwa "Almasi." Na wengine wao waliitwa "Bar X." Na wengine. . . Wetu walikuwa ni "Kiweko," kitu kama nembo ya Skauti wa Kiume. Jamaa huyo mwingine, chini yake, walikuwa ni "mburuzo wa batamzinga" juu ya farasi. Na wote walikuwa na chapa za kila namna, wa—wapate kuwajua ng'ombe wao walipowapeleka nje.

516 Sasa, mwangalizi hakuvutiwa sana na chapa waliyokuwa nayo, lakini jambo ni hili kwamba, mwangalizi alivutiwa na kuona kishikizo sikioni mwao. Kila kitu kilichoingia kule ndani, haidhuru kilikuwa ni cha chapa gani, kilipaswa kuwa ni cha asili bora ya Hereford. Hakingeruhusiwa kuingia kule isipokuwa kilikuwa ni Hereford. Ilibidi awe ni wa mifugo iliyosajiliwa la sivyo asingeweza kuruhusiwa kupita pale.

517 Nafikiri, kwenye siku ile wakati Bwana atakapokuja, Yeye hatajali tunavaa chapa gani, bali kwamba sisi sote ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo mifugo ya Kristo. Kipimo cha Damu kitatuthibitisha, sisi sote ni Wakristo. Na endapo sisi sote tutaenda kuwa hivyo *kule*, ni afadhali tuwe hivyo hapa. Je! hamdhani hivyo ndivyo itakavyokuwa? Hivyo ndivyo ilivyo, tunathamini ushirika wote kutoka kwenye makanisa yote mbalimbali.

518 Sasa tunajifunza kwenye Kitabu hiki kilichobarikiwa cha Waebrania. Ndugu mmoja amekifurahia sana hata amechukua kanda na anaandika kitabu cha mafundisho juu ya hiki.

519 Sasa tutakuja, hivi punde, kwenye mlango wa 11. Tunatarajia kupitisha majira ya baridi kwenye huo mlango wa 11. Kwa kila mmoja wa watu hao, tunataka kurejea nyuma kwenye Kitabu hiki kukipitia chote na kuunganisha Maandiko yote pamoja. Nilikuwa ninaenda kufanya jambo hilo. Ninafanya kwa sehemu, kwenye baadhi ya hii, ya hii milango iliyotangulia, nipate kukiunganisha Kitabu chote pamoja. Kwa maana, unaona, Andiko halina budi kuthibitisha Andiko.

520 Kwa hiyo, kama kuna kuhitilafiana kokote, ambapo mtu yeyote angefikiri ya kwamba Maandiko yanahitilafiana, hilo

ni kosa. Hakuna Andiko linalohitilafiana na Andiko. Hi—hitilafu ni pale ambapo kwamba labda yanahitilafiana na njia yetu ya kuliangalia, bali halijijipingi. Nimekuwa katika huduma, nikindelea kwa miaka ishirini na sita sasa, wala kamwe sijawahi ninii, wakati mmoja, kupata jambo moja katika Biblia linalopingana na jambo lingine lolote lililokuwa limeandikwa katika Biblia. Na ni—ninajua tu haliko.

521 Na leo tunajifunza katika moja ya milango iliyobarikiwa sana ya Waebrania, mlango wa 7. Na endapo kuna mtu asiye na Biblia, angetaka kutufuata katika haya tusomayo, tungefurahi kukuletea Biblia kama ungeinua tu mkono wako. Nitawaomba baadhi ya wazee hawa, mtu fulani, aje hapa na achukue hizo. Kuna watu wanainua mikono yao kule nyuma. Na asante, ndugu. Na iwapo unataka Biblia, inua tu mkono wako, nao watakuletea.

522 Sasa, njia pekee ambayo kanisa linaweza kujengwa, njia pekee ambayo mtu anaweza kupata Imani, si kwa njia ya madhehebu yake, wala kushirikiana nao. Hata hivyo Imani yake haikai juu ya theolojia ya mawazo ya mtu fulani, sababu hayo, takriban, ni mawazo ya mwanadamu kabisa. Bali njia pekee ambayo Imani inaweza kupata mahali pake thabiti pa kupumzikia, ni juu ya Neno imara na lisilobadilika la Mungu. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno." Hivyo ndivyo inavyokuwa. Na—na wakati Imani inaposikiwa na kukubaliwa, imetia nanga milele. Hakuna kitu kingine tena kinachoweza kuiondoa kamwe, hata kitu gani kitukie. Hakuna kitu kinachoweza kubadilisha Imani hiyo. Wazia jambo hilo. Umetia nanga, wala wewe hubadiliki tena, kwa wakati na Umilele. Umetia nanga milele, "Kwa kuwa Mungu, kwa dhabihu moja, amewakamilisha milele hao waliotakaswa, ama walioitwa."

523 Na imani ina nafasi kubwa sana katika Mkristo, maisha ya mwaminio, hivi kwamba inaweza kuchukua msimamo wake karibu na kaburi lenye matope ama juu ya jeneza, ambamo mtoto wa thamani ama mpenzi fulani ameyaacha maisha haya akaenda huko ng'ambo ya pili. Na kwa mtazamo mkali wa jicho la tai, inaweza kumwangalia Yeye aliyesema, "Mimi Ndimi ufufuo na Uzima." Nao wanasahau mambo yaliyo huko nyuma. Wanakaza mwendo kuifikilia mede ya wito mkuu.

524 Nina furaha sana ya kwamba Mungu ameitoa hiyo, na ameifanya kuwa karama ya bure kwa wote. Hivyo ndivyo makanisa yanavyopaswa kuwa. *Makanisa* halimaanishi madhehebu wala mashirika; inamaanisha, "Makundi ya watu, ya waaminio, ambao wamekusanyika pamoja chini ya ushirika wa Neno."

525 Na katika fundisho hili la ajabu sana hapa la Mtakatifu Paulo, katika misingi yake, katika milango iliyotangulia, yeye amekuwa akijiongelea maalum na Uungu mkuu wa Bwana Yesu

na kwamba Yeye alikuwa ni nani. Kristo alikuwa ni Mungu, aliyefanyika hivi kwamba wanadamu wangeweza kumpapasa na kumgusa, na—na kufanya ushirika Naye. Kristo, Bwana Yesu, alikuwa ni mwili ambamo Mungu aliishi, "Mungu alifanyika mwili na akakaa kwetu." Timotheo wa Kwanza 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili."

526 Yule Yehova mkuu alishuka na akafanyika aweze kugusika, kwa kuishi katika mwili wa Mwanawe Mwenyewe, akitangaza na kuupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Mungu hakuwa kitu. . . Kristo hakuwa kitu pungufu ya Mungu, wala—wala Mungu hakuwa kitu pungufu ya Kristo. Hao wawili pamoja walifanya Uungu kwa jinsi ya mwili, alifanywa punde mdogo kuliko Malaika, apate kuteseka. Malaika hawawezi kuteseka. Yesu alikuwa ni maskani ambayo Mungu aliishi ndani yake.

527 Biblia ilisema, katika mlango wa 7 wa Matendo ya Mitume, ya kwamba, "Maskani, na sadaka za kuteketezwa na dhabihu za kuteketezwa hukutaka, lakini mwili uliniwekea tayari. Hata hivyo Aliye Juu Sana haishi katika maskani zilizofanywa kwa mikono, bali mwili umeniwekea tayari," ili akae kwenye maskani au kuishi katika ushirika pamoja na mwanadamu.

528 Mungu akiruhusu, mara tutakapomaliza mlango huu hapa, ama kumalizia Kitabu hiki, tunataka kurudi na kukichukua Kitabu cha Ruthu na tuonyeshe mle ndani jinsi ambavyo Mungu alifanyika mtu wa jamaa yetu, apate kuwapatanisha waliopotea wamrudie Yeye Mwenyewe kwa kushiriki na kufanyika mmoja wetu. Mkombozi hana budi kuwa ni wa jamaa, na njia pekee ambayo Mungu angeweza kufanyika wa jamaa yetu, ni kufanyika mmoja wetu. Kwa hiyo, Yeye asingeweza kufanyika Malaika na awe wa jamaa ya mwanadamu.

529 Jana jioni wakati nilipokuwa nikizungumza na mwanangu aliyekuwa na huzuni nyingi, mwenzangu, juu ya mama huyo ambaye ndiyo kwanza aage dunia, alisema, "Lo Ndugu Bill, nadhani yeye ni Malaika usiku wa leo."

530 Nikasema, "Hapana, Earl. Kamwe hatakuwa Malaika. Yeye ni mwanamke, usiku wa leo, kama vile tu Mungu alivyomwumba, na atakuwa hivyo daima, sio Malaika kamwe." Mungu aliwaumba Malaika. Kamwe hakuwafanya wanadamu wawe Malaika. Yeye aliwaumba Malaika na wanadamu. Kwa hiyo wanadamu kamwe hawatakuwa Malaika, wala Malaika kamwe hawatakuwa wanadamu. Mungu aliwaumba tofauti.

531 Sasa, na Kristo kwa kufanyika mwili kukomboa kutoka katika hiyo ng'ambo kuu ambako mwanadamu alikuwa ameangukia, na kule kutopatikana na mauti kwa dhambi kulikuwa kumeshuka, Mungu alishuka na akachukua umbo la sura ya mwanadamu, na akawa ndugu yetu, ili Yeye apate kuchukua dhambi zetu na mauti yetu.

532 Na katika moja ya mifano tuliyokuwa tukitoa, katika masomo yaliyotangulia; msingi mdogo tu ili mgeni apate kuelewa. Mungu, akipanda kwenda Zake kule Kalvari. Ule mwiba wa mauti ukiwa juu Yake, na ulikuwa ukivuma kama nyuki kumzunguka, na hatimaye ukamchoma mpaka akafa. Alikufa mpaka jua likaacha kuwaka. Alikufa mpaka mwezi na nyota zingekoma kutoa nuru.

533 Ama, Yeye angefanyaje jambo hilo, ili auchukue mwiba wa mauti! Kama angalikuwa ni mtu asiyepatikana na mauti, kama angalikuwa katika theofani, ama angalikuwa katika roho, mauti hayana mamlaka juu ya huo. Ilibidi afanyike mwili, ili kwamba aweze kuutwaa mwiba wa mauti. Lakini wakati nyuki ama mdudu anayechoma mwiba, mara akididimiza ndani sana mwiba wake, kamwe hatachoma tena. Anauacha mwiba wake kwenye mwili huo. Na hivyo ndivyo Kristo alivyo-. . . ama Mungu alivyobadilika. Kristo aliishi katika mwili, apate kutwaa ndani ya mwili Wake Mwenyewe mwiba wa mauti. Na wakati mauti yalipojivuta yatoke Kwake pale msalabani, yaliacha mwiba wake, yasingeweza kumdunga mwamini tena. Yanaweza kutoa kelele za mvumo, yanaweza kuvuma kama nyuki na kutishia, bali hayawezi kudunga. Hayana mwiba.

534 Yule Mtakatifu mkuu Paulo, alipokuwa akielekea kwenye mauti yake, alipaaza sauti na kusema, “Ee mauti, u wapi mwiba wako? Na kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe ambaye tayari amekwisha kutupa ushindi kupitia kwa Bwana wetu Yesu Kristo, kwa kuwa mauti na kaburi vimepoteza nguvu zake.”

535 Sasa, basi, Jumapili iliyopita tulichukua, “Tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo,” katika mlango wa 6, tulisoma haya, “na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu.” Nasi tuliona ya kwamba watu siku hizi katika makanisa mengi, pamoja na maskani ya Branham na mengineyo, tunatilia mkazo sana juu ya kujifunza juu ya mafundisho ya kwanza ya Kristo: Yeye alikuwa ni Mwana wa Ibrahimu, alikuwa ni mwana wa—wa *fulani* wa *fulani,* na kurejea nyuma, zile koo. Lakini Biblia ilisema, “Na tuweke kando mambo hayo, na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu.”

536 Kwanza lazima ujue mafundisho, na halafu huna budi kujua mambo haya yote; halafu na tuyaweke kando, Yeye alisema, juu ya ufufuo wa wafu, kuwekea mikono, mabatizo, na sheria hizo zote za Mungu zisizo na uhai. Hata hivyo, ha—hazina Uzima ndani yao. Lakini kanisa siku hizi linayaendea tu mambo hayo, “Loo, tunaamini katika Uungu wa Kristo.” Naam. Hakika. “Tunaamini katika ubatizo wa maji.” Naam. Hakika. “Kuwekea mikono.”

537 Paulo alisema, “Tutafanya haya yote kama Mungu akiruhusu. Lakini mbele ya hayo yote, hebu na tuyaweke kando sasa, na tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu.”

538 Sasa, kanisa haliwezi kukamilishwa kupitia kwenye madhehebu. Linaenda mbali zaidi na Mungu, wakati wote, ama yanaachana mbali zaidi moja na lingine. Tunaweka mipaka, tunajitenga, inavyoelekea hatuna Imani. Lakini basi wakati tunapoacha kanuni hizo za mafundisho, kama tukikaza mwendo ili tuufikilie utimilifu, basi mambo hayo madogomadogo yanakuwa hayana umuhimu sana.

539 Tunaingia katika uhusiano, nasi tunaona ya kwamba njia pekee tunayoweza kukamilishwa ni kuwa ndani ya Kristo. Na ndipo tunaona basi, kwa mafundisho ya Biblia, ya kwamba jinsi tunavyoingia katika Kristo; si kwa ubatizo wa maji, si kwa kuwekea mikono, si kwa mafundisho. "Bali kwa Roho mmoja sisi sote tunabatizwa kuwa mwili Mmoja na tunakamilishwa kupitia mateso Yake." Ndipo, tunaonekana ni wa tofauti. Tunawazia tofauti. Tunatenda tofauti. Tunaishi tofauti. Si kwa sababu ni jukumu ama sisi ni wafuasi wa kanisa, bali ni kwa sababu ya "upendo ambao Mungu ameweka mioyoni mwetu kwa Roho Mtakatifu," ambao unatufanya raia washiriki pamoja wa Ufalme wa Mungu, ndipo hakuna madhehebu wala vizuizi katika jambo hilo. Sisi sote ni Mwili mmoja mkubwa.

540 Sasa tuko tayari kuingia kwenye somo la asubuhi, katika dakika chache. Jambo moja zaidi ningetaka kulifikia hapa, hilo ni, ya kwamba, Paulo akizungumza katika Kitabu hiki, cha mlango wa 7. . .ama mlango wa 6, hapa tunaona ya kwamba tunafanywa wakamilifu katika Kristo. Halafu katika kifungu cha 13 cha mlango wa 6, kwa kuweka msingi mdogo tu.

> *Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa sababu alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe wa kumwapa, aliapa kwa nafsi yake,*

Mungu aliapa kwa nafsi Yake, kwa sababu alikuwa hana mwingine yeyote mkubwa kuliko Yeye Mwenyewe wa kumwapa.

541 Sasa tunataka kurudi nyuma. Hebu na tufungue Wagalatia kwa dakika chache tu. Fungua kwenye Kitabu cha Wagalatia, na tufungue Wagalatia 3:16. Nasi tutasoma hapa mara moja, kwa kile alichoapia.

> *Basi* ahadi *zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, . . .Kwa mzao wako, yaani, Kristo.*

542 Sasa kama utaangalia, tukisoma hilo kwa makini sasa, unaposoma.

> . . .*ahadi* (wingi) *zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao* (umoja) *wake.*

543 "Ibrahimu na Mzao wake." Sasa, Mzao wa Ibrahimu ulikuwa ni mmoja, ambao ulikuwa ni Kristo; katika onyesho la awali, Isaka.

Lakini Ibrahimu alikuwa na watoto wengi. Yeye alikuwa na mmoja kabla hajampata Isaka, ambaye alikuwa akionyesha kupenyeza kwa kutokuamini kwa Sara ambaye alitaka Hana amzae mtoto huyo, akifikiri ya kwamba alikuwa ni mzee kupita kiasi, basi Mungu ilibidi akwepe na afanye njia nyingine mbali na njia aliyokuwa ameahidi kulifanya.

544 Lakini Mungu hushikilia ahadi Yake. Haidhuru huenda jambo lionekane lisilo la busara jinsi gani, Mungu anawajibika kwa ahadi Yake. Naye Sara alifikiri ya kwamba labda angeweza kumchukua Hana . . . ama Hajiri, hasa, mjakazi wake, amzalie Ibrahimu mtoto, na yeye Sara angemchukua. Na huyo akawa ni Ishmaeli, ambaye alikuwa ni kero ya mtu, tangu wakati huo hadi sasa. Angali ni kero, kwa maana kutokana na huyo walikuja Waarabu, nao wamekuwa hivyo sikuzote.

545 Sasa, wakati wowote unapoacha kuliamini Neno lililo dhahiri la Mungu na kuchukua njia fulani nyingine, itakuwa ni mwiba mwilini wako tokea wakati huo na kuendelea. Wewe chukua tu yale Mungu aliyosema. Kama alisema Hilo, hivyo ndivyo tu anavyomaanisha. Loo, Jina Lake na lihimidiwe! Chukua tu Neno Lake.

546 Haidhuru ni kitu gani kinachopita pembeni, kusema, "Vema, kweli halimaanishi Hivyo." Linamaanisha tu Kile lisemacho, wakati Mungu anapofanya ahadi.

547 Sasa kama tutaangalia kwa makini.

> . . . *ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake* . . .

Mmoja alikuwa ndiye huo Mzao, umoja, na huyo mwingine ilikuwa ni ahadi. Kuna ahadi zaidi ya moja, na mtu zaidi ya mmoja ambaye amehesabiwa katika Mzao wa Ibrahimu. Unaona? Kuna Mzao mmoja, bali watu wengi wa Mzao huu. Unaona? Hazikuwa tu ni kwa Ibrahimu peke yake, ama kwa Isaka peke yake. Lakini ninii . . . Ilikuwa ni kwa Mzao wote wa Ibrahimu. Ahadi zilifanywa kwa wote na kila mzao binafsi wa Mzao huo. Mnalipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

548 "Kwa hiyo, sisi, tukiwa wafu katika Kristo, kulingana na Maandiko, tunatwaa Mzao wa Ibrahimu na tu warithi kulingana na ile ahadi." Si kwa kujiunga na kanisa, ama kufanya matendo yasiyo na uhai, wala—wala na kadhalika. Bali ni kwa kuzaliwa na Roho wa Kristo, sisi ni Mzao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja Naye katika ule Ufalme.

549 Ndipo tunaendelea, kusoma, basi, mbele kidogo tu sasa, "Mungu akiapa." Sasa kifungu cha 17 cha mlango wa 6.

> *Katika neno hilo Mungu, akitaka* kuwaonyesha *zaidi sana* . . .

*. . .Mungu, akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati;*

550 Loo, hebu na tupumzike sasa dakika chache. "Mungu akitaka zaidi sana." Si kwamba ilimpasa kufanya hivyo, bali ni kulihakikisha jambo hili.

551 Sasa, tayari tumeona ya kwamba Mungu alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, jinsi ambavyo alijidhihirisha Mwenyewe kwa ulimwengu. Wakati alipompata yule mwanamke katika uzinzi, alisema, "Sininii. Sikuhukumu. Nenda, usitende dhambi tena." Wakati alipowakuta wagonjwa, alifanya vile vile tu ingembidi kufanya, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu, Naye—Naye aliwaponya wagonjwa. Alifufua wafu. Alisamehe dhambi. Haidhuru zilikuwa zikoje, na ni ngapi, na wao walikuwa wamerudi nyuma jinsi gani, Yeye aliwasamehe, hata hivyo, kama walikuwa wako tayari kuja na kusihi.

552 Sasa angalia. Kama Mungu alitenda wakati wowote kwenye hali fulani ya mambo, na kama hali iyo hiyo ikizuka tena, lazima atatenda mara ya pili kama alivyotenda mara ya kwanza la sivyo Yeye si mwenye haki. Unaona? Haidhuru wewe umezama jinsi gani katika dhambi, jinsi gani umeshuka, Yeye hana budi kutenda kwako kama alivyomtendea yule mwanamke aliyeanguka la sivyo alikosea wakati huo. Tabia ya Mungu ni Utu Wake, na vile alivyo katika matendo Yake kunaonyesha Utu Wake.

553 Na hivyo ndivyo ulivyo, katika matendo yako ya maisha, yanaonyesha kwamba wewe ni nani. Kama tulivyokuwa nalo na tulivyolipitia, somo moja ama mawili yaliyopita, Wamethodisti walitaka kusema, "Unapopaaza sauti, umempata." Mpentekoste anasema, "Uliponena kwa lugha, umempata." Mwenye Kutetemeka anasema, "Unapotetemeka, umempata," Watetemekaji wa Pennsylvania. Nasi tunaona ya kwamba wote wamekosea. Maisha yako yanatangaza jambo Hilo. Utu wako unaonyesha kwamba wewe ni nani. Mtu hujulikana kwa kazi zake, na chochote maisha yako yalicho.

554 Mmeisikia ile hadithi ya kale, "Maisha yako yanaongea kwa sauti kuu mno, siwezi kusikia maneno yako." Kwa hiyo vyovyote ulivyo, ndivyo ulivyo. Maisha unayoishi yanaonyesha ni roho wa aina gani aliye ndani yako.

555 Halafu tena, unaweza kuiga jambo baya. . .ama uige jambo zuri, hebu niseme. Unaweza kumwiga Mkristo. Lakini kutakuja, punde si punde, wakati ambapo majaribu yatakapoletwa, ndipo yataonyesha kwamba wewe ni nani. Nyororo ina nguvu zaidi kwenye kiungo chake kilicho dhaifu sana.

556 Wakati Kristo Mwana wa Mungu alipowekwa katika majaribio, ilionyesha kwamba alikuwa ni Nani. Hakika. Wakati unapojaribiwa, itaonyesha kile ulicho. Maisha yako daima

yanaonyesha kile kilicho ndani yako. Muda si muda, uwe na hakika dhambi yako haitakuumbua. Na hivyo ndivyo tunavyojaribu kusema.

557 Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye," si yeye atetemekaye, yeye anenaye. Yeye a-. . . "Yeye asikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hatakuja hukumuni; bali amepita toka mautini kuingia Uzimani."

558 Ni imani yako. Na imani yako, ikiungamwa kwa midomo yako, inadhihirisha kwa watu wanaoweza kusikia, bali maisha yako ni wazi mbele ya wote. Kwa hiyo, haidhuru unajaribu jinsi gani kutenda *hili* na kutenda *lile*, jambo hilo halitafaulu. Haina budi kuwa ndani yako. Hicho ndicho kiini halisi cha hadithi yote. Imani yako binafsi katika Kristo aliyefufuka, kama Mwokozi wako; ya kwamba yuko katika mkono wa kuume wa Mungu, akikuwakilisha asubuhi ya leo, kama vile unavyotenda mahali Pake hapa chini kama shahidi. Shahidi anapaswa kutenda badala ya mtu fulani, asimame kwa ajili yako kama shahidi. Na kama vile maisha yako yanaonyesha hapa kile ushuhuda wako ulivyo katika Kristo, yanaonyesha huko na yanaonyesha hapa. Naye yuko kule juu, kwa kuwa vile alivyo kwa ajili yako, inaonyesha sehemu zote mbili kule na hapa. Kwa hiyo wewe ni . . . Kwa imani yako, umeokolewa, na hiyo peke yake. Kwa hiyo, miamsho, mihemuko, hisia, kitu chochote kile, havina nafasi popote ndani Yake. Sasa, si . . .

559 Sasa, usiwazie vibaya, ya kwamba siamini katika mihemuko hii. Hakika ninaamini hawa. Lakini kile tunachozungumzia sasa, tunachojaribu kushindilia kwa watu wa siku hizi, si mihemuko. Ibilisi amechukua vitu hivyo na kuwapeleka watu mbali, akiwafanya waweke kikomo chao cha Milele juu ya mhemuko. Kupaaza sauti, kunena kwa lugha, kwenda kanisani kila Jumapili, kujifanya Mkristo, hilo halitasaidia hata kidogo kwenye siku hiyo. "Mtu asipozaliwa mara ya pili." Na maisha yako yanaonyesha kwamba wewe ni nani ndani, unaona, si mihemuko yako.

560 Ungeweza kuwa na damu mikononi mwako, ungeweza kunena kwa lugha, ungeweza kuwaponya wagonjwa, ungeweza kuihamisha milima kwa imani yako, na bado wewe si kitu. Wakorintho wa Kwanza 13. Unaona? Inabidi liwe ni jambo fulani lililotukia kwa Kuzaliwa ambako kunatoka kwa Mungu, na Mungu analeta Kuzaliwa upya ndani yako, na anakupa sehemu Yake Mwenyewe. Ndipo mambo hayo yanatendeka. Wewe ni kiumbe kipya. "Ninawapa wa Milele."

561 Tulipitia neno "Milele." *Daima* ni "kipindi cha wakati." *Milele* ni bila kikomo, daima na daima, bali kuna Milele moja tu. Nasi tunaona ya kwamba unapokea Uzima wa Milele, na neno hilo katika Kiyunani ni Zoe, ambalo linamaanisha "Uzima wa

Mungu." Nawe unapokea sehemu ya Uzima wa Mungu, ambalo linakufanya mwana wa kiroho wa Mungu, nawe ni wa milele tu kama Mungu alivyo wa milele. Huna mwisho, hakuna mahali pa kukoma, kwa kuwa hukuwa na mahali pa kuanzia. Kilicho na mwanzo kina mwisho, na kile kisicho na mwanzo hakina mwisho.

562 Jinsi tunavyolipenda Neno hilo la thamani! Jinsi ambavyo Mkristo anapaswa kuimarishwa katika Imani iliyokabidhiwa watakatifu mara moja, na wala asiyumbishwe huku na huko, mahali hadi mahali, na kujiunga na makanisa mbali mbali. Kanisa lolote unalotaka kujiunga nalo ni sawa, mradi tu wewe ni Mkristo. Lakini kwanza weka jambo la kwanza, ambalo ni kule Kuzaliwa kunakokufanya jamaa ya Mungu, kama vile Mungu alivyofanyika jamaa yako.

563 Yeye alifanyika ndugu, apate kukuinua. Kabla hajaweza kukuinua, hana budi kukupa Uzima wa Milele. Ndipo ilimbidi Mungu kufanyika wa jamaa yetu, apate kufa, ili akufufue. Basi inakubidi kuwa wa jamaa Yake, ili upate kuwa kwenye ufufuo. Unaona hicho ni kitu gani? Ni kubadilishana tu. Mungu alifanyika wewe, upate kufanyika Mungu. Unaona? Mungu alifanyika sehemu yako, mwili, upate kufanyika sehemu Yake kwa neema Yake, ni hivyo tu, upate kuwa na Uzima wa Milele.

564 Ni picha nzuri tu, na, lo, tunaipenda.

Sasa, *Mungu, akitaka kuwaonyesha zaidi sana . . .*

565 Haikumbidi kufanya hivyo, bali alikuwa tayari kufanya hivyo. Nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo, nawe je, ya kwamba Mungu wetu yuko tayari? Angalia. Vipi kama Yeye—vipi kama Yeye hakuwa mvumilivu? Tunda la Roho ni nini? Upendo, furaha, imani, amani uvumilivu. Hiyo ni sehemu ya Mungu iliyo ndani yako. Na inaweza kuvumilia, kuchukuliana mizigo mmoja kwa mwingine. Kusameheana, kama vile Mungu kwa ajili ya Kristo alivyokusamehe. Roho wa Mungu ndani yako anakufanya hivyo. Na ndipo Mungu alipokuwa hapa duniani na akawa wewe, akafanyika dhambi, hivi kwamba Yeye akazichukua dhambi zako, alizibeba kwa ajili yako na akalipa adhabu yako kwa ajili ya hiyo. Mungu ni mvumilivu, akichukua mizigo yetu.

566 Na kisha Yeye ni Mungu mwema. Ukitaka, mambo fulani kwa njia yako, unajua, Mungu ni mwema vya kutosha kufanya jambo hilo. Yeye anapenda ku—kukufurahisha. Anataka kukufurahisha. Yeye, Yeye ni upendo, na upendo Wake mkuu unamlazimisha hata kushuka wakati mwingine, kuacha upate vitu unavyotaka.

567 Mwangalie Tomaso, baada ya kule kufufuka. Tomaso hakutaka kuamini. Loo, yeye ana watoto wengi leo. Lakini Tomaso alisema, "La. La. Itabidi nipate ushahidi wa namna fulani. Itabidi niweke mikono yangu ubavuni Mwake, na

katika ninii Yake. . .vidole vyangu hapa kwenye mikono Yake, kabla ya kuamini Hilo. Mimi, mimi sijali mnasema nini." Unaona, alikuwa ametoka kabisa nje ya utaratibu wa Maandiko, papo hapo. Unapaswa kuyaamini Hayo. Kwa hiyo akasema, "Sina budi kuwa na namna fulani ya ushahidi, kuthibitisha jambo Hilo."

568 Ndipo Yesu akatokea, Yeye ni mwema, "Njoo, Tomaso, kama hilo ndilo unalotaka, vema, hili hapa. Unaweza kulipata."

569 Hivyo ndivyo tulivyo sisi. Tunasema, "Bwana, sina budi kunena kwa lugha. Si—sina budi kupiga makelele. Sina budi. . . "

570 "Loo, endelea, nitakuruhusu ulipate." Yeye ni mwema.

571 Kwa hiyo akaingiza mikono yake ubavuni Mwake, ndipo akasema, "Loo, ni Bwana wangu na Mungu wangu."

572 Akasema, "Sasa, Tomaso, wewe unaamini kwa kuwa umeona. Lakini ni kubwa zaidi sana vipi thawabu yao hao wasio na ushahidi na hata hivyo wanaliamini!" Haya basi. Hapo ndipo inapotubidi kufikia. "Ni kubwa zaidi sana vipi thawabu yao hao wasioona kitu bali hata hivyo Hilo wanaliamini." Ni tendo la imani, kwamba tunakubali jambo Hilo.

573 Sasa, mimi ninaamini ishara kufuatana na waaminio, lakini hebu na tuweke vitu vya kwanza kwanza. Unaweza kuwa na ishara, bila ya Hili. Paulo alisema ungeweza kuwa hivyo. Alisema, "Ningeweza kunena kwa lugha kama wanadamu na Malaika pia; si kitu mimi. Ninaweza kuhamisha milima kwa imani yangu; si kitu mimi. Ningeweza kuielewa Biblia, hivi kwamba ningeweza kujua siri zote za Mungu; si kitu mimi." Unaona, hizo ni karama za Roho Mtakatifu, bila Roho Mtakatifu.

574 Roho Mtakatifu ni Mungu. Mungu ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, subira. Huyo ni Roho wa Mungu. Hao ndio Mungu anaowainua katika siku za mwisho, kwa Roho huyo.

575 Sasa, "Asitake. . . "

> . . .*Mungu,* akitaka zaidi *sana kuwaonyesha zaidi sana warithio ile ahadi*. . .

> . . .*Mungu,* akitaka zaidi *sana*. . .*kuwaonyesha*. . . *warithio*. . .

Warithi ni akina nani? "Sisi, tukiwa wafu katika Kristo, tunakuwa Mzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi." Loo, hilo linakolea ndani? Sisi ni warithi wa Ufalme wa Mungu, kwa ahadi ya kiapo. Haikumbidi Mungu kuapa. Neno Lake ni kamilifu. Lakini Yeye aliapa, pia, kwa nafsi Yake, kwa kuwa hapakuwapo na mwingine aliye mkuu kuliko Yeye.

576 Tunapoendelea kusoma, hebu kidogo, sikilizeni.

> . . . ile *ahadi, jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, alitia kiapo katikati;*

577 "Yasiyoweza kubadilika," yule asiyebadilika. Mungu hawezi kubadilika. Hana budi kudumu vile vile. Na kama Mungu alimponya mgonjwa mmoja, Yeye kamwe hawezi kubadilisha nia yake. Mungu akimsamehe mwenye dhambi mmoja, kahaba mmoja, Yeye kamwe hawezi kubadilisha nia Yake. Kutokubadilika, kule kutobadilika kwa Neno la Mungu. Mungu alisema, katika mahali fulani, "Mimi ni Bwana anayeponya magonjwa yako yote." Hana budi kudumu Nalo, kwa maana Yeye hana kikomo. Alijua mwisho kutoka mwanzo.

578 Sasa, ninaweza kusema, "Nitafanya jambo *hili*." Nayo Biblia ilisema, tunapaswa kusema, "Bwana akipenda." Kwa sababu, mimi ni mwanadamu. Sijui. Wakati mwingine inanibidi kughairi neno langu, bali Mungu hawezi kughairi Lake. Yeye ni Mungu.

579 Naye aliomba jambo moja tu, "Kama unaweza kuamini." Loo, jamani! "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." "Kama unaweza kuamini," hilo tu. "Wewe, kama unaweza," hilo hapo swali. Bali swali lenyewe haliko kwenye Neno la Mungu, kwa sababu, Kutobadilika Kwake, Yeye hawezi kubadilika. Ni ajabu jinsi gani!

580 Sasa sikiliza, tunapoendelea kusoma.

> *Ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, . . .*

Haiwezekani! Kutowezekana na kutobadilika ni neno lile lile kwa kweli; haliwezi kubadilika, haliwezi kusogea. Halina budi kudumu vivyo hivyo milele. Haliwezi kubadilishwa, kutobadilika na kutowezekana.

> Na viwili*, ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, . . .*

"Tuna vitu viwili?" Naam. Cha kwanza, Neno Lake lilisema Yeye angefanya jambo hilo. Cha pili kilikuwa ni kiapo Chake alichoapa juu yake, kwamba Yeye angefanya jambo hilo. Loo, jamani!

581 Tunapaswa kuwa watu wa namna gani? Kwa nini turushwe-rushwe na kukimbia-kimbia hapa na pale, na kuchukua mambo ya ulimwengu na kutenda kama muundo huu laini wa Ukristo wa mwaka wa 1957? Tunataka kuwa wa aina ya mtindo wa kizamani ambao wanamchukua Mungu kwa Neno Lake, na kuviita vitu hivyo visivyokuwapo, kama kwamba vipo. "Kama Mungu alisema hivyo, Hilo latosha."

582 Ibrahimu, ambaye kwake hiyo ahadi ilitolewa, kwake na kwa Mzao wake, aliita vitu visivyokuwapo, kana kwamba vilikuwapo. Kwa kuwa, ilikuwa ni ahadi ya Mungu, akijua ya kwamba Mungu asingeweza kusema uongo. Yeye alimwahidi jambo hilo, naye aliliamini. Na miaka ilipoendelea kusonga

mbele, na ile ahadi ikawa kana kwamba inakuwa mbali zaidi, kwa jicho la kimaumbile, ilikuwa karibu zaidi kwa Ibrahimu.

583 Badala ya kuwa mdhaifu, na kusema, "Vema, labda hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Huenda nilikosea kutamka. Labda hakuna kitu kama hicho. Labda nimekosea katika mawazo yangu yote." Basi, hilo linaonyesha jambo moja, ya kwamba hujazaliwa mara ya pili. "Kwa kuwa ni . . . "

584 Tulipitia hayo Jumapili iliyopita, nyuma zaidi kidogo tu kwenye mlango huo. "Kwa maana haiwezekani kwa mtu ambaye amekwisha kuonja karama za Mbinguni na kadhalika, akianguka, kujifanya upya tena hata akatubu." Haiwezekani kabisa, kabisa!

> *Kwa kuwa yeye aliyezaliwa na Mungu* hatendi *na* hawezi *kutenda dhambi, kwa maana uzao wa Mungu* unadumu *ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi, . . .*

Uzao wa Mungu ni Neno la Mungu. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno, 'Dhabihu ilitolewa. Yote yamekwisha.'"

585 Sasa, kama ukifanya makosa, Mungu atakufanya uyajutie. Lakini ukifanya hivyo, umekosea, hufanyi hivyo makusudi. Mlango wa 10, kifungu cha 47, ninaamini, "Kwa kuwa tukifanya dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli." Lakini mara tu baada ya Kuzaliwa, unayo ile Kweli; si ujuzi Wake, bali umeikubali ile Kweli na imekuwa halisi. Nawe ni mwana wa Mungu, kwa wakati na Umilele. Mungu aliapa ya kwamba angefanya hivyo.

586 Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, Nami nitamfufua katika siku ya mwisho. Hatakuja hukumuni kamwe. Amepita toka mautini kuingia Uzimani." Sasa pamoja na kiapo cha namna hiyo, "Mungu akitaka ya kwamba tutaupokea."

587 Sasa angalia yale anayosema hapa, Paulo akiliambia ka— kanisa.

> *. . . Mungu hawezi kusema uongo,* tunapaswa kuwa na *faraja iliyo imara, . . .*

Si, "Vema, kama Wabaptisti hawatanitendea mema, nitakwenda kwa Wamethodisti." Unaona?

> *. . . tunapaswa kuwa na faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu;*

588 Sasa katika kusoma cha mwisho.

> *Matumaini tuliyo nayo kama nanga ya roho, . . .*

> Lile *tumaini,* kile kiapo alichoapa Mungu, *tuliyo nayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia;*

589 Hebu tuzungumze kidogo tu juu ya "pazia." Hatukulipata vizuri sana Jamapili iliyopita usiku.

590 "Ndani ya lile pazia." Pazia ni mwili. Pazia ndilo linalotuzuia kumwona Mungu, uso kwa uso, katika kanisa hili. Pazia ndilo linalotufanya tusiwaone Malaika kwenye nafasi zao asubuhi ya leo, wamesimama karibu na viti. Pazia ndilo linalotufanya tusimwone Yeye. Tumefichwa nyuma ya pazia, na pazia hilo ni mwili. Sisi ni wana na binti za Mungu, tupo Uweponi mwa Mungu, "Malaika wa Mungu wamefanya kituo kuwazunguka wale wanaomcha Yeye." Tupo Uweponi mwa Mungu, wakati wote. "Sitakuacha kabisa, wala sitakupungukia kabisa. Nitakuwa pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari." Lakini pazia hilo ni mwili, huo ndio unaotuzuia tusiwe katika Uwepo Wake. Bali kupitia kwa nafsi, Roho, kwa imani yetu tunajua ya kwamba Yeye anatuangalia. Anasimama karibu na sisi. Yeye yupo hapa sasa.

591 Kule Dothani, asubuhi moja, nabii mmoja mzee alikuwa amezingirwa na jeshi basi ndipo mtumishi wake akatoka na kusema, "Ee baba yangu, nchi yote imezingirwa na wageni."

592 Ndipo Eliya akasimama, na kusema, "Mbona, mwanangu, walio pamoja nasi ni wengi kuliko walio pamoja nao."

593 Vema, akapepesa macho yake na kuangalia pande zote. Hakuweza kuona kitu.

594 Akasema, "Mungu, natamani uyafungue macho yake, ondoa pazia." Ndipo pazia lilipoondolewa machoni pake, magari ya moto yalimzunguka huyo nabii mzee, milima ilikuwa ikiwaka Moto kwa Malaika na magari. Haya basi.

595 Loo, ndipo Gehazi aliweza kusema, "Na—nafahamu sasa." Unaona, pazia lilianguka. Hapo ndipo penye kizuizi.

596 Hili hapa. Lishikilie kwa dhati. Pazia ndilo linalotuzuia kuishi jinsi tunavyopaswa kuishi. Pazia ndilo linalotuzuia kufanya mambo tunayotaka sana kufanya. Naye Mungu akafunikwa na pazia la mwili, nalo pazia lilikatika vipande viwili. Ndipo Mungu akawa Mungu tena, Naye akainua pazia ambalo alijificha ndani yake. Huko ndiko kufufuka kwa Bwana Yesu. Akituthibitishia ya kwamba, katika pazia hili ambalo sasa tumefichwa ndani yake, kwa imani tunaliamini na kulikubali. Na wakati pazia hili litakapokatika vipande viwili, nitaenda kwenye Uwepo Wake nikiwa na uhakika huu, nikijua ya kwamba, "Ninamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake." Wakati wa Kuja kwa Bwana Yesu, pazia hili litafufuliwa tena, katika njia kamilifu, hata nitatembea na kuzungumza Naye kama Mwokozi wangu na Mungu wangu, hapo atakapokichukua kiti cha enzi cha Daudi. Nasi tutaishi milele katika pazia hili baada ya kukamilishwa, ila pazia hili lina dhambi ndani yake. Haijalishi vipi . . . Kamwe usiwazie juu ya huo mwili uliotukuzwa katika dunia hii. Hauna budi kufa,

vile vile ambavyo nafsi yako haina budi kufa, upate kuzaliwa mara ya pili.

597 Katika ule ukamilifu, si kula nyama, na kufanya *hivi*, na kuukamilisha mwili, hutakuwa nao kamwe. Na inakubidi kuacha *hili*, na kufanya *hivi*, na kufanya *hivi*, na kufanya *hili*, hiyo ni sheria. Hao ni wanasheria. Hatuamini katika taratibu za wokovu wa kisheria. Tunaamini ya kwamba kwa neema tumeokolewa. Wala si wewe. Huna uhusiano wowote na jambo hilo. Uteule wa Mungu ndio unaofanya jambo hilo. "Hakuna mtu anayeweza kuja kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Hiyo ni kweli. Naye... Yote aliyokuja kufanya Yesu yalikuwa ni kuwapata hawa ambao Baba alikuwa ametangulia kuwajua; na akawachagua tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Walifanyika wana na binti za Mungu. Amina. "Si yeye apigaye mbio, wala yeye atakaye, bali ni Mungu arehemuye." Mungu ndiye anayefanya jambo hilo. Huwezi kujivuna, hata kidogo. Hakuna kitu hata kimoja ulichofanya. Mungu, kwa neema, alikuokoa; si wewe, mwenyewe. Ukijiokoa, una kitu cha kujivunia. Bali huna kitu cha kujivunia. Sifa zote zinamwendea Yeye. Ni Yeye. Ndipo anakupa tumaini la hakika. "Aliapa kwa kiapo, kutowezekana kwa watoto Wake kupotea."

598 Sasa, wanapata mapigo kwa kufanya mabaya. Unavuna unachopanda. Unapata hayo. Usifikiri sasa utatoka tu nje na kutenda dhambi, ukwepe. Kama ukifanya hivyo, na una nia hiyo, inaonyesha wewe kamwe hujapata kuzaliwa mara ya pili. Unalipata? Kama ungali una shauku ndani yako, kufanya mabaya, basi ungali uko makosani. Unaona? "Kwa maana amewakamilisha, milele, hao ambao... Na hao wanyama chini ya lile Agano la Kale, chini ya siku za torati, walitolewa kila mwaka, daima, wasingeweza kamwe kuondoa dhambi." Lakini wakati tunapoweka mikono yetu juu ya kichwa Chake, na kutubu dhambi zetu na tuzaliwe mara ya pili na Roho wa Mungu, hatuna tena tamaa ya kufanya dhambi. Dhambi imekuacha. Hilo ni kwa wakati na Umilele.

599 Utafanya makosa. Utaanguka. Utafanya makosa makusudi. Utaondoka mara nyingine uende na kufanya mambo. Hilo halimaanishi ya kwamba umepotea. Hilo lina maana kwamba utarudiwa.

600 Mvulana wangu mdogo, mara nyingi, watoto wangu, watafanya mambo. Wako wanafanya, pia. Ya kwamba wewe... Wanajua hayo yanakiuka sheria—sheria zako. Nao wanajua cha kutarajia wanapofanya hivyo. Watapigwa viboko kwa kufanya hivyo, wakati mwingine viboko vikali. Bali angali ni mtoto wako. Hakika.

601 Haiwezekani kwa mtu huyo kupotea tena, akiisha kuzaliwa kwa Uzima wa Milele. Mungu si mpaji wa Kihindi. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka,

yuna Uzima wa Milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Nitamfufua katika siku za mwisho." Hiyo ni ahadi ya Mungu.

602 Sasa kama ukiendelea, useme, "Loo, vema, basi ninaweza tu kufanya . . . " Daima mimi hufanya ninachotaka kufanya. Bali kama wewe ni Mkristo, hutaki kufanya jambo baya, sababu ya Uzima wenyewe ulio ndani yako, msingi wenyewe. Iwapo unataka kufanya mabaya, inaonyesha kitu kibaya kiko hapa *ndani*. "Maji machungu na matamu yanawezaje kutoka katika chemchemi ile ile?"

603 Kwa hiyo nyote mmechanganyikiwa sana, kwenye namna fulani ya mhemuko ama mazingaombwe fulani, mhemuko mwingine. Sahau. Rudi madhabahuni na kusema, "Mungu, yaondoe maisha yangu ya kale yenye dhambi, na uniweke katika hali fulani ambapo shauku yangu yote . . . "

"Yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi." Hiyo ni kweli. Hana shauku ya kufanya hivyo.

604 Hakika, Ibilisi atamnasa *hapa* na *pale*, bali si makusudi. Biblia ilisema hivyo. Ibilisi atamnasa, mara kwa mara. Hakika, atamtega. Alijaribu kumtupia Bwana wetu Yesu mitego. Alimtupia Musa, na akamshika. Alimtupia Petro, akamshika. Aliwatupia wengi. Lakini Petro hata alimkana, bali baadaye alitoka akaenda akalia kwa uchungu. Kulikuwa na kitu fulani ndani yake.

605 Wakati hua alipoachiliwa atoke katika safina . . . Kunguru alipotoka, alilialia hapa na pale. Alikuwa kwenye safina kweli, bali alipotoka, tabia yake ilikuwa ni ya tofauti. Aliweza kula mizoga yote ya kale aliyotaka, na ashibe. Mbona? Yeye kwanza alikuwa ni kunguru. Alikuwa mla mizoga. Alikuwa hafai. Alikuwa ni mnafiki aliyeketi kwenye kiota pamoja na hua, akiwa mkubwa tu kama vile hua alivyokuwa. Angeweza kuruka kokote ambako hua angeweza kuruka. Lakini angeweza kula chakula kizuri kama vile tu hua alivyoweza kula. Na halafu pia angeweza kula chakula kilichooza, ambacho hua asingeweza kula. Kwa kuwa, hua ni wa kundi lingine. Ni wa maumbile ya tofauti. Yeye ni hua. Wala hua hawezi kumeng'enya chakula kilichooza, kwa maana hana nyongo yoyote.

606 Na mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu anakuwa hua wa Mungu, tabia yake, badiliko lake, maumbile yake. Naam, bwana. Ukiweka roho wa—wa hua ndani ya kunguru, kamwe hataketi juu ya mzoga uliokufa. Kama akitua juu yake kwa makosa, bila shaka ataondoka aende zake upesi. Asingeweza kuuvumilia. Na mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu, havumilii. Anaweza akaingia kwenye baa wakati mwingine, lakini atatoka humo upesi sana. Mwanamke anaweza akamshawishi, amfanye ageuke, bali atageuza kichwa chake tena. Ataondoka hapo upesi. Kwa nini? Yeye ni hua. Hiyo ni kweli. Hutampumbaza, kwa

sababu yeye anajua. "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu, wala mgeni hawatamfuata." Yeye kwanza ni hua, kwanza. Hilo ndilo ninalozungumzia, kitu halisi kinachotia nanga mle ndani.

607 Angalia kwa makini sasa. "Mungu aliapa." Loo, li- . . .

*Tuliyo nayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata—hata mle ndani ya pazia,*

608 "Pazia." Mungu alishuka, akajificha nyuma ya pazia la mwili. Kufanya nini? Kujionyesha Mwenyewe. Ilibidi ajifiche, kwa maana tusingeweza kumwona. Naye alijificha nyuma ya pazia. Na pazia ilikuwa ni nani? Yesu. "Si Mimi ninayefanya hizo kazi, Baba Yangu," alisema Yesu. "Baba Yangu anakaa ndani Yangu. Ninatenda kazi. Baba anatenda kazi, Nami ninatenda kazi hata sasa." Huyu hapa kama aliyetiwa utaji, akitembea katika mwili, Mungu, Imanueli, Mungu pamoja nasi. "Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Huyu hapa, akitembea mahali pote.

609 Sasa, Yeye alishuka na kufanya utakaso, ama akifanya utaratibu, au upatanisho, ili kwa toleo la mauti Yake, alilipa gharama ya dhambi, apate kurudi na kukaa ndani yetu. Ndipo imani tuliyo nayo ni—ni imani iliyotiwa utaji, ama mtu aliyetiwa utaji. Kwa hiyo hatuangalii mambo tunayoona katika utaji huu. Utaji huo una elimu mbalimbali, na unafanya mambo pia huzungumza mambo. Ni mtambo wa kisayansi. Lakini Roho wa Mungu aliye hai anayeishi hapa ndani, huita vitu hivyo ambavyo havikuwapo, kana kwamba vilikuwapo, kama Mungu alisema hivyo. Huko hapo kutiwa utaji kwako. Tuko wenye utaji.

610 Sasa, siku moja Yeye atauinua utaji huu, si uliozaliwa na mwanamke kwa tamaa ya kujuana kimwili ya mwanamume na mwanamke, bali kwa mapenzi ya Mungu atanena na itatimia. [Ndugu Branham alidata kidole chake—Mh.] Ndipo tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe uliotukuzwa. Tutakuwa tumetiwa utaji, tupate kuzungumza mmoja kwa mwingine, tupeane mikono.

611 Sasa, tunapoondoka kutoka hapa, kuna maskani, theofani, sura tu ya mwanadamu, ambayo haili, hainywi, hailali, inakaa macho milele. Huko ndiko tunakoelekea. Bali wao wanangojea chini ya Madhabahu, wakilia, "Bwana, hata lini? Hata lini?" washuke kurudi huku chini. Kwa sababu, wanataka kupeana mikono mmoja kwa mwingine. Wanataka kuketi na kula, na kuzungumziana. Wao ni wanadamu. Jina la Bwana libarikiwe!

612 Mungu alipomfanya mtu katika sura Yake hapo mwanzo, Yeye alimfanya jinsi hii. Alifanya ushirika mmoja kwa mwingine, kwa maana tunafahamiana. Tunapenda yale mambo ambayo Mungu alitufanyia, kwa kuwa tulifanywa hivyo. Katika kule Kuja Kwake kukuu, wale walio tayari watakuwa hivyo milele. Tutabaki katika sura Yake, tusiopatikana na mauti. Lo! hilo Jina la Kristo na lihimidiwe!

613 Na sasa tuna arabuni ya wokovu wetu, tunapomkubali Yeye kama Mwokozi wetu binafsi, kama mponya wetu. Tunzo hizi zingine zote ni marupurupu yanayolipwa kwenye hati ya bima. Amina. Unajua hati ya bima ni kitu gani. Unaweza kupata marupurupu kwake mpaka ufikie kwenye thamani yake halisi. Hakika. Unaweza kupata marupurupu. Nasi tunapata marupurupu sasa. Ila tu, jambo ni kwamba, mara tunapopata marupurupu, hesabu inaongezeka tena.

614 Mwanabima, wakati mmoja, aliniambia, "Billy, ningetaka kukuuzia bima."

Nikasema, "Ninayo." Mke wangu akaniangalia.

615 Sasa, sina kitu dhidi ya bima. Lakini watu wengine ni "maskini wa bima." Kwa hiyo, wakageuka. Akasema . . .

616 Mke wangu akaniangalia, kwa mshangao, "Ati una bima?"

617 Nikasema, "Hakika." Hakuwa na habari yoyote kuhusu hilo.

618 Yule mtu akasema, "Vema, Billy, una bima ya aina gani?"

619 Nikasema:

Ndiyo dhamana, Yesu wangu!
Hunipa furaha za mbingu!
Mrithi wa wokovu wangu,
Nimezawa kwa Roho Yake.

620 Akasema, "Hilo ni jambo zuri sana, Billy," akasema, "bali haitakuweka hapa makaburini."

621 Nikasema, "Lakini itanitoa. Hilo ndilo jambo muhimu." Mimi sina wasiwasi wa kuingia mle; nina wasiwasi wa kutoka.

622 Na kwa kuwa nina hiyo bima, kwa kiapo cha Mungu wa Milele, ya kwamba atanifufua tena katika mfano wa Mwanawe, katika siku ya mwisho, nitatembea kwa ujasiri na kuwa na faraja na kuwa na nanga ya nafsi, hivi kwamba, nikiwa katika utaji huu kuna kitu Fulani kisichoonekana kilichonitia nanga kwenye Mwamba wenye imara huko ng'ambo. Wakati maji yanaporuka na kulipua mshindo, haileti tofauti yoyote. Kama mauti, hatari kubwa, ama chochote kile, hakitutenganishi na upendo wa Mungu. Nanga yangu inashikilia kwenye pazia. Acha mafuriko yainuke. Acha yafyatuke. Acha makafiri waje. Mwamini aliyezaliwa mara ya pili ana nanga. Huwezi kuangalia kupitia kwenye pazia hili bado. Lakini ninajua nanga yangu inashikilia huko kwenye Mwamba wenye imara, ambaye ndiye ahadi ya kiapo ya kwamba atanifufua siku ya mwisho.

623 Si ajabu unaweza kuiangalia mauti usoni, na kusema, "U wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Bali Mungu na ashukuriwe atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Tuko ndani ya yule Mtangulizi. Loo, jamani! (Hatutafikia kwenye somo.) Tulikuwa na Mtangulizi kwa ajili yetu.

624 Mtangulizi. Je! uliwahi kuona katika zile siku za kale za magharibi. Mara nyingi nimepitia kwenye ile miburuzo ya zamani. Mtangulizi, ama skauti? Wakati gari lililokokotwa na farasi lilipokuwa linaangamia, kwa kukosa maji, skauti alitangulia mbele mbio. Naye akawaona makabila ya Wahindi; akayapita. Na akaona mahali palipokuwapo na chemchemi ya maji. Alirudi nyuma mbio kumwambia bosi wa hilo gari la farasi, "Wachapuze farasi, kila mtu na ajipe moyo, kwa kuwa pale juu tu ya mlima kuna chemchemi kubwa ya maji." Yeye ni mtangulizi.

625 Na huyu hapa, yule Mtangulizi. Binadamu wakati mmoja alikuwa akibanwa chini na Ibilisi, chini ya mashambulizi makali sana, lakini mtu Fulani alichukua bombomu kubwa. Huyo alikuwa ni Yesu. Mtangulizi ametutangulia. Na Shetani amesimama pale na bombomu, akitubana chini, daima tukiwa utumwani na kuhofu mauti. Alikuwa akilinda Chemchemi hiyo. Hakika, alikuwa akiilinda. Alipewa agizo, kwa kuwa tulikuwa tumetenda dhambi na tukafukuzwa toka Huko. Lakini Mtangulizi, Kristo, aliingia na kuchukua ile bombomu.

626 Mmeusikia ule wimbo wa zamani, "Shikilia ngome, kwa maana Mimi ninakuja"? Shikilia ngome, hakuna kitu; hebu na tuiteke. Hatutaki kuishikilia zaidi. Kristo aliiteka hiyo ngome. Haleluya! Mlango umefunguliwa. "Kuna Chemchemi iliyofunguliwa katika nyumba ya Mungu, katika mji wa Daudi, kwa ajili ya kutakasa, kwa ajili ya utakaso wa wasio safi." Mtangulizi wetu tayari ameingia ndani kwa ajili yetu.

627 Mtangulizi, Yeye anatwambia, "Kuna mahali fulani hapo ng'ambo tu, ng'ambo ya pili, ambako hutakuwa mzee kamwe." Ambako hakutakuwako na makunyanzi, ambako haitakubidi kutumia vipodozi vya Max Factors kukufanya uonekane mzuri kwa mume wako. Mtangulizi ametangulia. Kuna mahali ambako kamwe hutazeeka na kuchoka na kutetemeka. Kuna mahali ambapo kamwe hutakuwa mgonjwa. Ambako mtoto mchanga kamwe hatasokotwa na tumbo. Ambapo kamwe hutatoa ninii ya bandia . . . ama jino, kuweka la bandia. Haleluya! Loo Jina Lake libarikiwe! Yeye aliingia, nasi tutadumu daima wasiopatikana na mauti katika sura Yake, siku moja huko ng'ambo. Watang'ara kuliko nyota na jua. Hakika. Mtangulizi ametutangulia.

> *. . . alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu. Amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki.*

628 Mtangulizi huyu mkuu ametutangulia, akitufanyia njia. Alitoka katika roho, zile chemchemi kuu za upinde wa mvua wa Mungu, ambaye hakuwa na mwanzo wala mwisho. Yeye alikuwa, milele, Mungu.

Mwali huu wa Nuru ulitoka. Ulikuwa ni mwali wa upendo, huo ndio ule mkubwa, mwekundu. Rangi nyingine inayofuata, ambayo ilikuwa ni ya bluu; bluu, ukweli. Mwingine, ulioufuata

huo ulikuwa ni rangi zingine, kupitia zile rangi saba kamilifu, ambazo ni roho saba za Mungu, zilizotoka kwenye Chemchemi hiyo kuu ama ile Almasi kuu ambayo Yesu alinena habari zake. Hiyo Almasi kuu ilikatwa, ipate kuakisi rangi hizi. Mungu alifanyika mwili na kukaa kwetu, apate kuakisi wema Wake na rehema miongoni mwetu, kwa karama na ishara na maajabu.

Upinde wote huo mkubwa wa mvua ulikuwa umekuwa theofani, iliyofanywa kwa mfano wa mwanadamu. Hata hivyo, Yeye hakuwa ni mwanadamu; hakuwa na mwili, bado. Alikuwa ni theofani.

629 Musa alisema, "Ningetaka kukuona." Mungu akamficha katika mwamba.

630 Ndipo wakati alipopita hapo, aligeuza mgongo Wake. Musa akasema, "Ulionekana kama mgongo wa mwanadamu."

631 Halafu ni kitu gani kilikuja kutukia? Siku moja kule, wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi hemani mwake. Tutafikia jambo hilo, usiku wa leo. Wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi hemani mwake, Mungu alimjia, katika mwili wa nyama.

"Loo," unasema, "Ndugu Branham, yeye alikuwa . . . "

632 Tutamkuta huku akikutana na Ibrahimu kabla ya hapo, kwa mfano wa Melkizedeki, mwili wa nyama, ambao ulikuwa ni Mungu. Hakika, alikuwa mwili wa nyama. Alikuwa ni Mungu katika mwili.

633 Unasema, "Basi, Ndugu Branham, kwa nini basi ilimlazimu kurudi na kuzaliwa?"

634 Hakuwa amezaliwa wakati huo. Alikuwa tu ameumbwa, mwili alimokaa. Melkizedeki alikuwa ni Mfalme wa Salemu, ambaye ni Mfalme wa Yerusalemu, ambaye ni Mfalme wa amani; ambaye hakuwa na baba wala mama, mwanzo wa siku zake wala mwisho wa uhai wake.

Yesu alikuwa na baba na mama pia, na mwanzo wa siku Zake na mwisho wa uhai Wake. Bali alifanywa "kwa mfano wa" Melkizedeki, ambaye hakuwa na mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa uhai Wake.

635 Melkizedeki alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Melkizedeki alikuwa ni Yehova Mungu, yeye Yule aliyekutana na Ibrahimu, miaka kadhaa baadaye, mbele ya hema lake. Alikuwa amemwelekezea mgongo Wake; akasema, "Kwa nini Sara amecheka?" Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa ndiye aliyesimama pale, akielekeza uso Wake Sodoma. Ibrahimu alimtambua, kwa maana ndani ya pazia lake kulikuwako na nanga iliyoshikilia ile ahadi. Si kwa sababu alikuwa na mhemuko fulani, bali Mungu alimpa ahadi. Na wakati alipogusana na ile sumaku kuu, alijua ilikuwa ndani ya ule mwili.

636 Akatoka akaenda pamoja na Ibrahimu, huko nje mahali fulani hatua chache. Akamwambia Ibrahimu. Akasema, "Kwa

kuwa, je! nitamficha Ibrahimu mambo haya, kwa kuwa yeye ni mrithi wa dunia? Sitafanya hivyo kamwe." Kwa hiyo, "Ibrahimu, nitakwambia kile ninaenda Zangu kufanya," tutalichukua hilo usiku wa leo, "huko Sodoma," na yale wote waliyokuwa wanaenda kufanya. Na mara alipokwisha kumbariki Ibrahimu, alirudi katika anga tena. Mtu aliyesimama pale na alikuwa na mavumbi nguoni Mwake, mwanadamu. Na si hayo tu, bali alikula nyama ya ndama ambaye Ibrahimu alimchinja, na kunywa maziwa toka kwa ng'ombe, na kula keki chache (ugali kidogo), na zilipakwa siagi. Hiyo ni kweli kabisa. Na kisha akageuka akarudi kwenye theofani tena.

637 Ilikuwa ni kitu gani? Kwa nini hakuchukua wakati ule? Yeye hakuwa kamwe amezaliwa kama mimi na wewe. Lakini ilibidi azaliwe katika mwili, apate kushikilia mwiba huo. Huo ulikuwa ni mwili ulioumbwa. Huo ulikuwa ni mwili ambapo alitwaa tu kalisi na potashi kutoka kwenye udongo, na kusema, "Whiu," na akaingia ndani yake. Hicho ndicho kitu kile kile Melkizedeki alichokuwa. Aliingia ndani yake, katika mwili ambao angeweza kutembea mbele zake chini ya pazia, pazia la uumbaji Wake mwenyewe; si utaji wa uumbaji wa mwanamke, kupitia katika tumbo la uzazi la mwanamke, kupitia se—seli, la hasha. Lakini aliuumba huu na kuingia ndani yake, na kuzungumza, akiwa katika mfano wa Melkizedeki.

638 Je! huyu Melkizedeki ni nani?

> *Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa Salemu,* (ambao ni Yerusalemu), mfalme *wa Mungu aliye juu,* hakika, *aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki;*
>
> *Ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote; tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki,* (ule upendo mkuu, upendo, yule Roho mkuu hapo mwanzo) . . . *mfalme wa haki, tena, Mfalme wa Salemu, maana yake, Mfalme wa amani;*
>
> *Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, . . .*

639 Alikuwa ni nani? Kamwe hakuzaliwa, hatakufa kamwe. Ni nani? Ilikuwa ni Mungu, hakika, ilikuwa hivyo, katika kuonyeshwa mbele kwa Bwana Yesu. Hakika alikuwa hivyo. Bali ilibidi aje kupitia kwa mwanamke, kama vile wewe unavyopitia kwa mwanamke. Naye ilibidi aje jinsi ulivyokuja, kusudi akurudishe Kwake. Haleluya!

> Neema ya ajabu sana, jinsi inavyosikika tamu,
> Iliyomwokoa maskini, fukara kipofu kama mimi!
> Nilikuwa nimepotea, bali sasa nimepatikana, kwa neema Yake,
> Nilikuwa kipofu, bali sasa naona.

640 Ninafahamu kile alichopaswa kufanya. Mungu alifanyika mimi, kusudi mimi kwa neema Yake niweze kufanyika Yeye. Aliondoa dhambi zangu, kusudi mimi kwa haki Yake nipate Uzima wa Milele. Nisingeweza kuchagua mimi mwenyewe. Asili yangu ilikuwa ni mwenye dhambi. Sikuhusika kwa chochote na jambo hilo. Nilizaliwa "na binadamu, nikaumbika katika maovu, nikaja ulimwenguni nikisema uongo." Sina hata na uwezekano, hata kidogo; sina cho chote, sina hata shauku.

641 Mwambie nguruwe ni "makosa, kula takataka," sivyo? Uone atakusikiliza kiasi gani. Mwambie kunguru ni "makosa, kula mzoga uliokufa," na uone vile atakavyokwambia. Kama angeweza kuzungumza, "Shika lako." Hakika.

642 Loo, bali neema ya Mungu iliyobadilisha asili hii, na kunipa mlango wa kupenda na kuwa na shauku na kuona kiu, "Upendo wako, wema, ni bora kwangu kuliko uzima, Ee Mungu. Moyo wangu utakuonea shauku."

643 Daudi alisema, "Kama vile ayala akioneavyo shauku kijito cha maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea kiu, Ee Mungu."

644 Mungu alimpa mwanadamu hiyo kiu, kumwabudu, kumpenda, kumtafuta. Lakini mwanadamu anaipotosha kwa ombi la Ibilisi, naye anaenda na kuwatamani wanawake na anasa na mambo ya dunia, akijaribu kuridhisha uumbaji huo mtakatifu ambao Mungu ameweka humo ndani, kumpenda Yeye. Anauweka juu ya mambo ya ulimwengu. Lakini, ndugu, mara mtu anapobadilishwa, na hiyo chemchemi iliyo na vifurukuta mikia ndani yake, kila namna ya—ya machafuko ya birika hilo, imesafishwa na bakteria wameondolewa, na Maji masafi ya Mungu yametiwa mle ndani, dhambi haiwezi kamwe kuyagusa. Amina.

> Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomwabudu!
> Uzima wangu, mwanga wangu wa jua, yote katika yote kwangu!
> Huyo Muumbaji mkuu alifanyika Mwokozi wangu,
> Na utimilifu wote wa Mungu unakaa ndani Yake.
>
> Alishuka kutoka utukufuni Mwake, ndiyo hadithi iishiyo daima,
> Mungu wangu na Mwokozi wangu alikuja, na Yesu lilikuwa ndilo Jina Lake.
> Alizaliwa horini, kwa walio Wake akawa mgeni,
>
> Mungu wa huzuni, machozi na uchungu mkali.

Loo jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyomsujudu!
Pumzi yangu, mwanga wangu wa jua, yote kwa yote kwangu!

645 Ee Mungu! Aliwezaje kufanya jambo hilo? Mwanadamu amejaribu kuuandika huo. Mmoja alisema:

Kama tungaliijaza bahari kwa wino,
Na kila shina duniani lingalikuwa ni kalamu,
Na mbingu zote zimetengenezwa kwa karatasi;
Na kila mtu awe kazi yake ni mwandishi;
Kuandika upendo wa Mungu aliye juu.

Jinsi huyo Mungu mkuu wa Mbinguni alivyofanyika mwili na akazichukua dhambi zangu!

Kuuandika upendo wa Mungu aliye juu
Kungeikausha bahari yote;
Ama ingawa gombo hilo lingechukua nafasi yote,
Hata kama limetandazwa kutoka mbingu hadi mbingu.

646 Na kuwafanyia warithi wa wokovu huu tumaini la hakika, Yeye aliapa kwa nafsi Yake ya kwamba angetufufua katika siku za mwisho, atupe Uzima wa Milele. "Wala hakuna mtu anayeweza kuwatoa mkononi Mwangu." Amina.

Na tuombe.

647 Je! wewe una hatia ya kudharau upendo Wake? Je! umeukataa Utu Wake uliotukuka, Huyu Mwenyezi aliyekufanya jinsi ulivyo? Na sasa uko hapa, asubuhi ya leo, umbali huu maishani, na inakupa nafasi. Je! unataka kuendelea kuishi? Kuna njia moja tu ya kuishi, hiyo ni kumwamini Bwana Yesu. Kama wewe, kutoka moyoni mwako, unaamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu na umkubali kama Mwokozi wako, na uamini ya kwamba Mungu alimfufua upate kuhesabiwa haki, kama unataka kukubali jambo hilo kwa msingi huo, jambo hilo ni lako sasa.

648 Ungeweza kuinua mkono wako? Mtu yule ambaye hajatubu, ambaye angetaka kuninii...-tubu, kutubu asubuhi ya leo, aseme, "Nikumbuke, ndugu, mhubiri, tunapoingia katika maombi. Mimi pia nimeshindwa. Nimejiunga na kanisa, lakini na—najua kamwe si—sijawahi kuwa na hayo unayonena habari zake. Sijawahi kuzaliwa kwa Roho huyo, Ndugu Branham. Si—sina tu Huyo, hivyo tu. Ninataka uniombee, ya kwamba Mungu atanipa Hilo asubuhi ya leo." Mungu akubariki, bwana. Je! kungekuwako na mwingine? Aseme, "Mungu, nifanye jinsi unavyotaka mimi niwe. Ninataka Wewe uwe...Ninataka kuwa jinsi unavyonitaka mimi niwe. Nimepuuza upendo Wako." Mungu akubariki, mwanangu.

649 Hebu kidogo tu, sasa.

Kama tungaliijaza bahari kwa wino,
Na kama mbingu zote zimetengenezwa kwa karatasi;
Kama kila shina duniani lingekuwa ni kalamu,
Na kila mtu awe kazi yake ni mwandishi;
Kuuandika upendo wa Mungu aliye juu
Kungeikausha bahari yote;
Ama kama gombo hilo lingechukua nafasi yote,
Hata kama limetandazwa kutoka mbingu hadi mbingu.

Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo tajiri na msafi!
Jinsi usivyopimika na una nguvu!
Utadumu milele,
Wimbo wa watakatifu na Malaika.

650 Mungu mpenzi, hakika mshairi aliyeandika maneno hayo alikuwa tu kama wengine wengi wa waaminio Wako, akitafuta, akijaribu kupata maneno ya kulielezea. Na imeandikwa katika Biblia, "Zaidi, kwa sababu mhubiri alikuwa na hekima, alichunguza na kuweka maneno mengi katika utaratibu." Loo, jinsi tungependa kuwa na lugha na msamiati ambao tungeweza kuwaelezea watu kwamba ni kitu gani hasa, bali hayangeweza kupatikana katika midomo ya mwanadamu. Milele yote, hakuna shaka kama itaweza kuufunua, jinsi ambavyo Mungu wa Mbinguni aliwahi kushuka duniani kuwaokoa maskini fukara, wenye dhambi, waliopotea.

651 Ninakuomba, Baba, ya kwamba kupitia kwenye haya maneno machache yasiyovunjika-vunjika, ama maneno yaliyovunjika-vunjika asubuni ya leo, kama nilivyopaswa kusema, ya kwamba mtu fulani amepata amani na ridhaa na faraja yenye nguvu, ambaye amekimbilia mahali pa salama. Na jalia nafsi yao itie nanga kwenye hiyo ahadi ambayo Mungu aliiapia, ya kwamba angewafufua katika siku ya mwisho. Mikono kadhaa iliinuliwa, hapa jengoni, papa hapa katika maskani hii. Mungu, wape hilo tumaini imara, sasa hivi. Jalia watie nanga kwenye Mwamba wenye imara. Haidhuru bahari itapiga mawimbi jinsi gani na ya jahazi yao yaruke-ruke jinsi gani, wao wana nanga, ahadi ya Mungu. Hapo wao wanashikilia, "Mungu alinena Hilo. Hawezi kusema uongo."

652 "Yeye ayasikiaye maneno Yangu," ambalo nimejaribu kuhubiri asubuhi ya leo, "na kumwamini Yeye aliyenipeleka, Yehova, yuna Uzima wa milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani."

653 Ewe wa Milele, wabariki hao leo. Na jalia kila mtu hapa ndani asiye chini ya Damu hiyo, nafsi yao haijawahi kuongoka,

jalia itukie sasa hivi, Bwana. Fanya muujiza. Yote ni Yako. Limekabidhiwa Kwako. Naomba ya kwamba utawapa hilo, Uzima wa Milele. Jalia, siku moja, huko kwenye pwani ya pili, wakati tukipitia bondeni mmoja mmoja, jalia tukutane kule ambako kamwe hawatasema tena "kwa heri."

> Siku moja tutakuja mtoni wakati wa kumalizika kwa wakati,
> Wakati mawazo ya mwisho ya huzuni yamepita;
> Kutakuwako na mtu fulani akingojea ambaye atatuonyesha njia,
> Haitanibidi kuvuka Yordani peke yangu.
> Kutakuwako na Mmoja, mtu fulani akingojea ambaye atanionyesha njia,
> Haitanibidi kuvuka Yordani . . .

654 Wote walio na tumaini hilo, inua mkono wako sasa unapoinua kichwa chako.

> Haitanibidi . . .

Sasa hebu mwabudu tu. Ujumbe umekwisha. Je! hamna furaha? Mungu aliapa asingeninii . . . Mungu aliapa atakutana nanyi kule.

> Yesu alikufa apate kulipia dhambi zangu zote;
> Wakati giza ni- . . .

Unasemaje? Mwiba umeondoka.

> Atakuwa akiningojea,
> Haitanibidi kuvuka Yordani peke yangu.

> Mara nyingi ninaachwa, na ni mchovu . . .

Mwabuduni tu sasa.

> Inaonekana kana kwamba marafiki wangu wote wameondoka;

Je! ulipata kufikia mahali hapo?

> Bali kuna wazo moja linalonichangamsha.

Hiyo ahadi ilikuwa ni nini?

> Inaufurahisha moyo wangu,
> Haitanibidi kuvuka Yordani . . .

655 Sasa, enyi wana wa ahadi, hebu mwabuduni tu kwa kufanya jambo hilo.

> Haitanibidi kuvuka Yordani peke yangu,
> Yesu alikufa apate kulipia dhambi zangu zote;

Inakuwaje sasa?

> Nitakapoona lile giza, Yeye atakuwa akiningojea,
> Haitanibidi kuvuka Yordani peke yangu.

"Nitakapofika mtoni." Kila mmoja wenu anakuja. Kuna kivuli kikubwa, cheusi, kilicho pale mbele yenu. Ni mlango mkubwa. Unaingia humo ndani, moja ya siku hizi, labda kabla siku haijaisha, labda kabla kanisa halijafungwa asubuhi ya leo. Unaingia humo. Kila mara moyo huo unapopiga, wewe uko hatua moja karibu zaidi.

> Lakini nitakapoona lile giza, Yeye atakuwa akingoja pale,

Alisema ataningojea. Aliapa ataningojea.

> Basi haitanibidi kuvuka Yordani peke yangu.

656 Ee Bwana mbarikiwa, mioyo yetu imejaa, asubuhi ya leo, hata kufurika.

657 Kuwazia juu ya wakati pigo la moyo linapokoma, na nesi anasukumiza foronya kichwani mwako. Na mikono yako, huwezi kusogea tena. Mikono yako imekuwa barafu. Watoto wako, mama yako, wapendwa wako wanaomboleza na kulia. Ule mlango mkubwa unafunguka, huko ng'ambo. Yeye atakuwa akingoja.

658 Daudi alisema, "Kama nikifanya kitanda changu katika kuzimu, Yeye atakuwa huko." Haitanibidi kuuvuka peke yangu. Wakati manyunyu ya mto yatakapoanza kurukia usoni mwetu, Mungu atachukua mashuaokozi, atuongoze moja kwa moja tuuvuke. Aliahidi atafanya hivyo. Nabii Daudi alisema, "Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa maovu. Wewe u pamoja nami. Fimbo yako na gongo lako, vyanifariji."

659 Bwana, tuna furaha sana leo, ya kwamba tulihesabiwa warithi wa ile ahadi. Leo tuna Uzima wa Milele ndani yetu, kwa maana tunampenda Bwana Yesu na tumemwamini, na tumelikubali Neno Lake na mafundisho Yake. Naye alitupa, kama muhuri wa imani yetu, Roho Mtakatifu, muhuri wa Roho Mtakatifu. Imani yetu ndani yetu imetiwa nanga. Na ingawa mara nyingi tunatembea kupitia kwenye vivuli vyeusi, mara nyingi tunajikwaa barabarani, lakini nanga yetu ingali bado inashikilia. Kuna kitu fulani ndani yake, huko ng'ambo ya mbali, kinachoonekana kikiongoza, kikisema, "Songa mbele. Tunasonga mbele."

660 Mungu, tubariki. Tunakuhitaji. Tudumishe kuwa waaminifu na wa kweli mpaka wakati utakapokuja kutuchukua, tutakushukuru katika nyakati zote zisizo na mwisho. Na siku ile wakati tutakaposimama duniani. . . Miguu yake mitakatifu haijawahi kukanyaga duniani bado. Yule pale amesimama pale, hewani; na watakatifu na waliokombolewa kutoka katika nyakati zote, kupitia katika kila zamu, ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, na ya saba, wote watasimama pale wamevikwa haki Yake; tutamvika taji Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, na kuimba zile hadithi za ukombozi. Maskini mioyo yetu itatetemeka tutakapomtazama

Yeye aliyetupenda na akajitoa kwa ajili yetu. Tulipokuwa tusiopendeka na wenye dhambi, Kristo alikufa kusudi tupate kuokolewa. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Baba, katika Jina la Kristo. Amina.

661 Mnampenda? Loo, jinsi alivyo halisi. Je! hivi hamjisikii kana kwamba mngetaka tu kwa namna fulani kumkumbatia Yeye kwa mikono yenu? Hivi msingependa sasa hivi kutambaa kumwendea na kuigusa miguu Yake, unajua?

662 Unajua, kulipata kuwa na watu waliokuwa wakija kwenye ibada zangu huko Phoenix, Arizona, wakisema, "Ningetaka kuwa na mazungumzo ya pamoja Naye. Ningetaka kusema, 'Bwana, ulinipenda wakati njia yangu ilipoingia utusitusi mkubwa.'" Ningependa tu kuwa na mazungumzo ya pamoja Naye kabla hatujavuka. Ni—ninataka tu kumwona Yeye. Na—na—nataka tu kumwona. Kuwazia jinsi vile nitakavyojisikia, jinsi maskini moyo wangu utakavyotetemeka nitakapomwona Yeye amesimama pale.

663 Mara nyingi nimeshangaa, "Laiti ningaliweza kusikia Sauti hiyo ikisema, 'Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo. Nitawapumzisha.'"

664 Labda kamwe sitasikia hayo dhahiri kama alivyoyanena wakati huo, bali ninataka kumsikia akisema, "Hii ndiyo siku ya mwisho. Ulifanya vema, mtumishi wangu mwema na mwaminifu, sasa ingia katika furaha za Bwana zilizoandaliwa kwa ajili yako." Tangu lini?

665 "Tangu ulipookolewa?" La, ndugu.

666 "Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati nilipokuona na kukujua tangu zamani, na kukukusudia Uzima wa Milele," ulibarikiwa wakati huo. "Wote aliotangulia kuwajua, Yeye aliwaita." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] "Wote aliowaita, Yeye aliwahesabia haki. Wale aliokwisha kuwahesabia haki, tayari amewatukuza." Haya basi. Yeye alitangulia kutujua, akatuita, akatuhesabia haki, na tayari tumetukuzwa pamoja Naye, katika mwisho wa dunia, tukienda kupata tuzo letu. Hivi hamna furaha? ["Amina."] Hakika. Mtu ingekufanya kumpenda. Wakati usingeweza kujisaidia, Naye huyu hapa akaja na kufanya jambo hilo kwa ajili yako.

667 *Kibarikiwe Kifungo Kiifungayo*, Dada Gertie. "Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo," wakati tukiwa na ushirika huu mdogo hapa sasa wa kuabudu, halafu tutaenda kuwaombea wagonjwa. Mungu awabariki. Ninyi mliomwinulia Kristo mikono yenu asubuhi ya leo, jitafutieni mahali pa kuabudia, mkamtumikie.

668 Sasa, hebu na tumwabudu tu sasa, kama kusanyiko, ninyi Wamethodisti wote, kanisa la Mungu, Assemblies of God, Wapresbiteri, Walutheri, Katoliki. Sote pamoja sasa, hebu na tuimbe sasa.

Kibarikiwe kifungo kiifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa ndugu wenye nia moja
Ni kama ule wa Mbingu.

Mbele ya kiti cha enzi cha Baba,
Twamimina maombi yetu ya motomoto;
Hofu zetu, tumaini letu, makusudio yetu, ni mamoja,
Faraja yetu na wajibu wetu.

Tufumukanapo,
Moyo unaumia;
Lakini bado tungali tutaunganika katika . . .

Ni Wamethodisti wangapi, Wabaptisti, na kadhalika?

Tena twatamani kukutanika tena

669 Je! hilo haliwafurahishi? Hebu na tugeuke na kupeana mikono sisi kwa sisi sasa, wakati tukiuimba huo tena.

Mbele . . .

Peaneni mikono, na mtu wa nyuma yako, mbele yako, pande zote mbili.

. . . kiti cha enzi,
Twamimina maombi yetu ya motomoto;
Faraja zetu na fadhaa zetu.

Sasa tufumukanapo,

Tutapendana sisi kwa sisi.

Hilo linatupa . . .

Mngetaka sana kama ibada ingaliendelea? Unaona? Hivyo ndivyo tunavyofikiri.

. . . unaumia;
Lakini tungali pamoja rohoni kuwa kitu kimoja,
Na tunatumaini kukutana tena.

Tusipokutana hapa tena, kwenye ile Siku kuu tutakutana.

670 Sasa, Baba, pokea ibada yetu asubuhi ya leo. Chukua Neno na ulipande ndani ya mioyo ya waaminio. Jalia wasirushwe-rushwe hata kidogo, na leo wamepanda juu na kesho wameshuka chini, bali jalia maneno haya yapate mahali pa kupumzika katika kila moyo wa mwaminio. Kujua jambo hili, ya kwamba, "Mungu ameapa kwa kiapo, na kuna mambo mawili yasiyoweza kubadilika. Kutobadilika kwa Mungu, hiyo ni kusema, ya kwamba haiwezekani Yeye kusema uongo, ya kwamba warithi wa wokovu huu wapate kuwa na tumaini hili lenye nguvu, lililo imara na la hakika, nanga ndani ya nafsi." Kujua jambo hili, ya kwamba, "Mungu ametuahidi, kwa kiapo kilichoapiwa. Jambo moja, ni kwamba Yeye hawezi kusema uongo; lingine, aliapa kiapo juu ya hilo, ya kwamba atatufufua katika siku ya mwisho

na kutupa Uzima wa Milele." Tukijua jambo hili, ya kwamba, "Tukiisha kuitwa, ya kwamba Yeye alisema ya kwamba alitujua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kutuchagua tangu zamani tupate kufanywa wana wenye mamlaka kwa Yesu Kristo. Naye alitujua tangu zamani. Akatuita. Na wakati alipotuita, Yeye alituhesabia haki." Hatuwezi wenyewe kujihesabia haki, kwa hiyo Yeye alituhesabia haki kwa mauti ya Mwanawe Mwenyewe. "Hao aliowahesabia haki, tayari amewatukuza." Neno limenenwa tayari. Nasi tuko tu njiani, tukienda zetu, tukiwa wa njiani huku tukifurahia tukielekea Utukufuni.

671 Wape watu imani, na jalia tabia ndogo-ndogo na kadhalika ambazo zimewashika watu, jalia zipukutike ziwaondoke, asubuhi ya leo, kwa Neno hili la Mungu ambalo ni nanga ya nafsi, iliyo imara na ya hakika. Jalia waachane na tabia zao, hasira zao ndogo-ndogo. Na mambo yaliyopita. . .Kama vile Paulo alivyosema, katika sehemu ya mbele ya ujumbe siku chache zilizopita, "Na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; tupate kupiga mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu; tukimtazama mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, Yesu Kristo, ambaye alijaribiwa kwa kila hali kama tunavyojaribiwa, bali bila ya kutenda dhambi." Yeye aliruhusiwa kujaribiwa, bali hakuanguka majaribuni. Nasi tunajaribiwa kutenda dhambi, bali katu hatutii hilo. Kwa kuwa Uzima ulio ndani yetu ni nanga ya kikomo chetu cha Milele, nasi tunashikilia hilo likiwa baraka moyoni mwetu.

672 Sasa, kuna wengi ambao Shetani amewatesa kwa mateso. Tunajiandaa kuwaombea, Baba. Jalia wao, wakati wanapopita chini ya Neno la Mungu leo. . .Hilo Neno la thamani ambalo limehubiriwa, Biblia ikitoa ushahidi, Malaika wa Mungu wakisimama karibu, na yule Roho Mtakatifu mkuu, juu ya yote, anasimama hapa kulishuhudia Neno. Sasa, Baba, wanapopitia chini ya Neno la ahadi asubuhi ya leo, jalia waondoke toka hapa waende wakapate afya. Wakavue vyuma vyao vya miguuni, wakaondoke kwenye viti vyao na—na machela wanayolalia, na wakafanywe wazima kabisa. Tujalie hayo, Bwana. Wajalie warudi kwenye ibada ijayo ambayo watajaliwa kuja, ama wakifurahi huko kwenye makanisa yao, wakidhihirisha mambo makuu ambayo Kristo amefanya. Haya tunayahudumia kwa ajili ya utukufu Wako, katika Jina la Yesu. Amina.

673 Ninapaswa kuomba msamaha kwa ajili ya ahadi niliyotoa, ya kwamba asubuhi ya leo tungechukua mlango wa 7, lakini sikuufikia. Na inatupasa kuruhusu muda kidogo hapa kwa ajili—kwa ajili ya jambo hili, kwa ajili ya mstari wa maombi. Na sasa, usiku wa leo, Bwana akipenda, tutachukua mlango wa 7, na tuone huyu Melkizedeki alikuwa ni nani. Ni wangapi wangetaka kujua? Loo, tunashuka moja kwa moja kwenda Kwake, tupate

kujua kwamba Yeye ni nani hasa. Na Maandiko yanaelezea kwamba Yeye ni nani. Unaona?

674 Na Scofield alisema ilikuwa ni "ukuhani." Ingewezekanaje kuwa ni ukuhani, bila mwanzo wala mwisho? Unaona, haikuwa ni ukuhani. Ilikuwa ni Mtu, Melkizedeki (jina), Mtu.

675 Kama vile, si kupuuza, lakini Christian Science linasema ya kwamba Roho Mtakatifu ni "wazo." Na Biblia ilisema, "Yeye, Roho Mtakatifu." Na *Yeye* ni kiwakilishi nafsi. Ni Mtu, si wazo. Ni Mtu. Kweli kabisa.

676 Naye Melkizedeki ni Mtu, Mtu ambaye hakuwa na mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa miaka Yake. Hakuwa na baba wala mama, wala wazazi. Nasi tutaona kwamba Yeye ni nani, Bwana akipenda, usiku wa leo, kwa Neno. Je! mnalipenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo! "Neno Lako ni taa katika njia yangu na miguu yangu." Loo!

677 Sasa, unasema, "Ndugu Branham, silielewi Hilo lote." Wala mimi pia.

678 Lakini, wakati mmoja, nilikuwa nikihubiri huko Kentucky. Na kwa baadhi ya wageni, na Wakatoliki na watu mbalimbali, ambao huenda wasifahamu mambo haya yenye kilindi, yaliyokolea ya Maandiko. Nimekuwa nikihubiri juu ya uponyaji wa Kiungu. Maskini msichana mdogo asiye na viatu akaletwa . . . Hakuwa na umri wa miaka kumi na tano, alikuwa na mtoto mchanga, naye alikuwa na ugonjwa wa kutetemeka mwili. Nikasema, "Mtoto wako ana shida gani, dada?"

679 Akasema, "Yeye ana mishtuko." Hakujua la kusema, kutetemeka mwili. Hakujua jina la huo.

680 Maskini msichana huyo labda hajawahi kuvaa jozi ya viatu, maishani mwake. Kipenzi cha mwanamume fulani, nywele ndefu zikining'inia chini. Nikasema, "Je! unaamini?"

681 Ndipo hayo macho madogo, ya kijivu ya feleji yakaniangalia. Akasema, "Ndiyo, bwana. Hakika ninaamini."

682 Nikamchukua maskini mtoto huyo mchanga. Na wakati nilipokuwa nikimwombea, aliacha kutetemeka. Aa. Ndipo akatoka, akatoka.

683 Kesho yake, nilikuwa nikiwinda kindi, upande wa pili wa mteremko wa mlima. Nikawasikia watu wameketi kule wakizungumza, huo msumeno wa tangu na tangu ukivuma. Nami nikanyemelea kwenda kule walikokuwa. Nilikuwa katika kuwinda kindi. Walikuwa wakizungumza habari zangu, wameketi pale, wakitafuna tumbaku na kutema mate. Matawi yakipepea, namna hiyo. Nao walikuwa wakizungumza kuhusu, sasa, kuhusu mkutano wa usiku uliopita. Mmoja wao akasema, "Nilimwona huyo mtoto mchanga. Nilipitia karibu na pale, asubuhi ya leo. Angali hatetemeki, asubuhi ya leo." Unaona?

Wakasema, “Lile lilikuwa ni jambo halisi.” Naye alikuwa akitema mate.

684 Nao walikuwa wameegemeza bunduki kwenye mti, kwa hiyo nikawazia bora nijitambulishe. Mwajua, walikuwa na uhasama kule, pia. Kwa hiyo, nikaenda pale. Nikasema, “Habari za asubuhi, ndugu zangu.”

685 Yule jamaa mkubwa mno, alionekana kana kwamba anazungumza, alikuwa anatafuna tumbaku mdomoni mwake, namna *hiyo*, huku chini upande mmoja namna *hiyo*, mwenye shingo kubwa, ndefu. Naye alikuwa amevaa kofia kubwa mno iliyochakaa, imevutwa chini kwenye uso wake. Aliangalia kule niliko akaniona. Akanyosha mkono na kuishika hiyo kofia, akaivua upesi, akafanya . . . [Ndugu Branham anameza—Mh.] Akaimeza hiyo tumbaku ya kutafuna, kasema, “Habari za asubuhi, mchungaji.” Unaona? Naam, bwana. Heshima. Na hiyo ni kweli. Jinsi alivyostahimili jambo hilo, sijui, bali aliimeza.

686 Kwa hiyo, usiku uliofuata, nilipokuwa nikirudi, kulikuwako na mtu pale aliyetaka kubishana na mimi kidogo. Alihudhuria kanisa ambalo haliamini uponyaji wa Kiungu. Basi, hili lilikuwa ni kanisa la Kimethodisti, White Hill, Kentucky. Kwa hiyo a— akaenda kuninii . . . Alikuwa amesimama nje. Alikuwa na taa ya kandili mkononi mwake. Basi akasema, “Ninataka kusema jambo fulani, mhubiri. Siwezi kabisa kukubali jambo Hilo, maana siwezi kuliona.”

687 Nikasema, “Huwezi kuliona?”

688 Akasema, “La.” Kasema, “Mimi mwenyewe ni mgonjwa. Lakini,” kasema, “Siwezi kuliona kabisa.”

Nikasema, “Unaishi wapi?”

Akasema, “Huko mbali kwenye Big Renox.”

Nikasema, “Vema, utafikaje nyumbani?”

Akasema, “Vema, nitaenda nyumbani kwa miguu.”

Nikasema, “Je! unaweza kuona nyumba yako?”

Akasema, “La, bwana.”

Nikasema, “Kuna giza sana usiku wa leo, kuna mawingu.”

Akasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Utakwendaje nyumbani?”

Akasema, “Kwa taa hii.”

Nikasema, “Hiyo kandili haiangazi kote njia nzima mpaka nyumbani.” Nikasema, “Utaendaje?”

Akasema, “Loo, ninatembea kwa taa hii.”

689 Nikasema, “Sawa kabisa. Una nuru ya taa sasa, na kila mara unapopiga hatua upande *huu*, nuru hiyo itaendelea kumulika mbele yako. Kama ukiendelea tu kutembea, nuru hiyo itaendelea kwenda pamoja nawe.”

690 Nawe fanya hivyo asubuhi ya leo, ukimtaka Kristo, yule Kuhani Mkuu, Mwombezi wa maradhi yako, ama magonjwa yako, ama nafsi yako. Huenda usifahamu jambo Hilo. Hatulifahamu. Bali tumeamriwa “Kutembea katika Nuru kama vile Yeye alivyo katika Nuru.” Unapiga hatua moja katika Nuru. Na unapokuwa na hiyo Nuru, Nuru hiyo itaangaza hadi siku ile kamilifu. Itamulika njia mbele zako.

> Nasi tutatembea kwenye barabara hii kuu,
> Nikitangaza kokote niendako,
> Afadhali niwe Mkristo wa mtindo wa kale, Bwana,
> Kuliko chochote nijuacho.

Umepata kusikia wimbo huo wa kale?

> Hakuna kitu kizuri kama Mkristo wa mtindo wa kale,
> Kuonyesha upendo wa Kikristo;
> Tunatembea kwenye ile barabara kuu ya kale,
> Na kutangaza mahali pote twendako,
> Afadhali niwe Mkristo wa mtindo wa kale, Bwana,
> Kuliko chochote nijuacho.

691 Ninapenda tu kuwa hivyo. Vema. Sasa tutawaombea wagonjwa. Sisi si-. . . Hatudai ya kwamba tunaweza kuwaponya wagonjwa. Kama tungedai hivyo, tungekuwa tukisema uongo. Kila mtu aliye mgonjwa hapa ndani ameponywa tayari. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema. “Kwa mapigo Yake tuliponywa.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

692 Kila mwenye dhambi aliyepo hapa ndani, labda kungekuwako na mmoja, umeokolewa tangu Yesu alipokufa. Lakini kamwe usife hapa ambapo nafasi yako iliwekwa mbele zako, kuingia katika Uwepo Wake kisha kujaribu kuukubali. Hilo limefanywa kwa ajili ya wakati huu. Sasa hivi unapaswa kuukubali. Kama ukivuka Damu, basi wewe si kitu ila. . . Tayari umehukumiwa, kwa kuwa unahukumiwa kwa vile ulivyoutendea Upatanisho wa Bwana Yesu Kristo. Unaona? Wewe, unajihukumu pale.

693 “Kwa hiyo alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa mapigo Yake sisi tumeponywa.” Kwa hiyo, hakuna kitu ningekuwa nacho, cha kukuponya wewe. Hakuna kitu kanisa lingekuwa nacho, cha kukuponya. Kitu pekee tunachoweza kukiombea ni hiki, ya kwamba imani yako haitashindwa, ya kwamba utakuja madhabahuni asubuhi ya leo na kumkubali Kristo kama Mponya Wako, kama ulivyofanya kuwa Mwokozi wako. Na bila ya ninii yoyote. . . Mungu hufanya miujiza. Yeye huonyesha ishara kuu. Vipofu, viziwi, bubu, kila kitu, wanaponywa papa hapa maskanini. Lakini kama wanaponywa ama hawaponywi,

tunakubali jambo Hilo, hata hivyo. Mara nyingi vitu hivyo ni kwa maono.

694 Ni wangapi waliokuwapo hapa yapata Jumapili tatu zilizopita, ama nne, wakati mtu yule alipoingia hapa, akiwa kipofu na amepooza, ama ameketi kwenye kiti akiwa ni mwenda wazimu. Na kabla sijaondoka nyumbani, nilimwona katika ono, "Ya kwamba kutakuwako na mtu kule, mwenye nywele nyeusi, zimeanza kuwa na mvi. Mke wake ni mwanamke mwenye umbo zuri, mwenye umri wa karibu miaka sitini. Atakuja na atakuwa akilia," naye ataniomba. "Na nirudi nikamwombee mumewe." Huyo mumewe aliketi pale pale.

695 Ndipo nikaja. Nikawaambia baadhi ya ndugu zangu hapa, "Angalieni jambo hili."

696 Na wakati tuliposhuka kwenda madhabahuni, wengine walikuwa wameomba. Nilipoenda kuomba, nilienda zangu moja kwa moja na kurudi hapa. Ndipo mkewe akaamka na akaja vile vile kabisa Bwana alivyokuwa amesema ingekuwa. Watu wakiangalia, waone kama ingetukia vivyo hivyo. Haijakosea kamwe. Na kwa hiyo wakati huyo mtu alipotembea . . .

697 Nikaja kuona, ya kwamba mtu fulani, Dkt. Ackerman, kule Birdseye, Indiana, alikuwa ndiye aliyemtuma aje hapa; ambaye ni Mkatoliki, na mvulana wake ni padre kule katika nyumba ya watawa ya Mtakatifu Meinrad. Naye Dkt. Ackerman ni mwindaji mwenzangu, naye alimtuma mtu huyo kuja hapa. Ndipo Bwana akanionyesha mtu mwenye nywele nyeusi ambaye angemtuma, bali sikujua alikuwa ni nani.

698 Nikasema, "Je! huyo alikuwa ni Dkt. Ackerman?"

699 Akasema, "Ilikuwa ndiye." Unaona? Na ndipo mtu huyo . . .

700 Nikasema, "Ni BWANA ASEMA HIVI." Nikashuka nikaenda. Nikasema, "Bwana, simama." Ni kipofu na pia asingeweza . . . yeye . . . Ne—neva ya akili timamu ilikuwa imekufa. Asingeweza kujishikilia namna hiyo. Unaona? Amekuwa hivyo kwa miaka mingi, amekwenda kwa akina Mayo na kila mahali. Ndipo nikamwombea ombi tu, na nikamwinua. Huyo hapo akaenda, akishuka kwenda zake.

701 Kwanza akasema, "Siwezi kukuona." Kisha akapiga makelele, "Ndiyo. Ninaweza." Macho yake yakafunguka pale. Alikuwa ni mwothodoksi, mke wake ni Mpresbiteri.

702 Watu wengine wanafikiri ya kwamba "Mpresbiteri hapaazi sauti kwa nguvu, na Mwothodoksti." Laiti ungaliwasikia. Ni kweli. Walikuwa wakipiga makelele na kukumbatiana. Akarudi na kuchukua kiti chake chenye magurudumu, na akapanda akitoka na kushuka kwenye vipandio, kama vile tu mtu mwingine yeyote, angeweza kuona na kuongea na—na kadhalika.

703 Nilipata barua kutoka kwake, ama nilimpigia, hivi majuzi. Ninaamini Ndugu Cox alienda kwake. Kasema, “Macho yake yalikuwa na mwasho mkali.” Hakika. Ni ile neva, neva za macho zinaota na kupata uhai, unajua, na kuchukua mahali pake. Laana iliondolewa.

704 Kama utaachilia maumbile yafanye yatakavyo, kama hakuna kitu kinachoyazuia maumbile, basi yata—yatafanya yapendavyo. Kama una bendeji mkononi mwako, likizuia mzunguko wa damu, mkono wako hatimaye utakufa. Sasa, kwa sababu, kimaumbile, utakuwa sawa kama utauachilia tu. Lakini kitu fulani kimeyakatiza maumbile. Basi, kama huwezi kuona jambo hilo, hakuna njia kwa daktari kulipata. Kuna vitu viwili tu anavyoweza kutenda kazi navyo: kile anachoweza kuona na kile anachoweza kuhisi. Hiyo ndiyo njia pekee anayoweza kutenda kazi nayo: kile anachoona na kile anachohisi.

705 Kama hawezi kukiona, basi hakina budi kuwa ni cha kiroho. Ndipo kuna ninii, jambo pekee liwezalo, jambo moja linaloweza kutendeka; tunaomba, Kristo anaondoa laana hiyo, anamtoa Ibilisi, na huo unaanza kuwa wa kawaida, kupona. Anakuwa mzima, na ni hayo tu. “Katika jina langu watatoa pepo.” Hiyo ni kweli? Ni ahadi waliyopewa kanisa. Ni ahadi ya nguvu. Ati nini? Huo, ni Uwepo Wake pamoja nasi. Sasa, kile kinachotufanya tusikamilike asubuhi ya leo, kufanya mambo hayo kama tu Yeye alivyoyafanya, ni kwa sababu tungali tuko katika pazia. Unaona? Lakini tuna hisi fulani pale inayotwambia, “Loo, ndio.” Unaona?

706 Na wakati unapokubali uponyaji wako. . .Haidhuru pazia linasema nini, ni kile Neno lilichosema. Unaona? Naam. Ndiyo hayo. Na Ne—Ne—Neno daima lina mamlaka juu ya chochote. Neno la Mungu la Milele!

707 Mwangalie Sara, tumbo lake la uzazi limekufa, umri wa miaka tisini, aliishi na mumewe tangu alipokuwa na umri wa miaka kama kumi na sita ama kumi na saba, hawana watoto; Ibrahimu, mia moja. Mungu aligeuka moja kwa moja na akawapa mtoto. Unaona? Kwa sababu, waliamini. Waliviita vitu hivyo ambavyo havikuwa, kana kwamba vilikuwapo. Ingia kwa jinsi hiyo asubuhi ya leo, rafiki.

708 Na usiku wa leo, tunatarajia. . .Kama ninyi nyote mnatutembelea, tuna furaha kuwa pamoja nanyi hapa asubuhi ya leo. Na Mungu awe pamoja nanyi. Na kama uko humu mjini jioni ya leo, tungefurahi kuwa pamoja nawe jioni hii ya leo kwenye ibada hii iliyosalia, ya Melkizedeki. Na tena kama hutakuwapo, na una kanisa lako mwenyewe, nenda kwenye kanisa lako. Hilo—hilo ndilo jukumu lako mwenyewe. Kama wewe ni mfuasi wa kanisa, nenda kule. Hii ni maskani ndogo tu ambapo tunakusanyika hapa ndani na kufanya ushirika sisi kwa sisi. Sasa, Bwana awabariki.

709 Naye Dada Gertie atatupigia wimbo, *Ni Tabibu wa Karibu*. Na kuna yeyote hapa wa kuombewa? Inua mkono wako, wale wanaotaka kuja kwenye mstari wa maombi, kuweka imani yako kwa Kristo. Vema. Kama mtafanya mstari upande huu wa kanisa, mkiweza. Na kama watasogeza viti chini kidogo tu, ndugu, tafadhali, ili kwamba tupate nafasi kidogo mle ndani na tunaweza kuwapitisha watu. Njoni upande *huu*.

710 Nasi tutaomba sasa, wakati tunapoimba. Nami nitawaomba wazee wa kanisa hapa, wa madhehebu yoyote ama kanisa, haidhuru ni lipi, kama mnaamini katika uponyaji wa Kiungu, je! mngeweza kusimama pamoja nami hapa jukwaani, kuwaombea wagonjwa? Tutafurahi kuwa pamoja nanyi. Madhehebu yoyote, ama bila madhehebu, ama chochote ulicho, tutafurahi kuwa pamoja nawe. Tafadhali njoni tu sasa, kwa ajili ya maombi, njoni hapa na msimame pamoja nami.

Ndugu Neville, naomba uje na mafuta.

*KITABU CHA WAEBRANIA*

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org